Nipashe
MWANGA WA JAMII
Alhamisi Juni 25, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580267
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

Albinism Hotline
• Jifunze kuhusu Ualbino
• Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino
0800 75 00 50
Piga simu bure
HAKI YETU PROJECT
UNDER THE SAME SUN
215779502



## Maiti za vichanga zapotea kiajabu hospitali ya mkoa

UKURASA 3

# Lowassa na mkewe wamdhamini JPM

UKURASA 2



## MCHIMBAJI MDOGO ALAMBA BIL. 7/-

UKURASA 2

Mchimbaji mdogo wa madini ya Tanzanite, Saniniu Laizer, akiwa na mawe makubwa mawili ya madini hayo kabla ya kumkabidhi Waziri wa Madini, Doto Biteko (kushoto), baada ya kuiuzia serikali kwa Sh. bilioni 7.7, katika Mji Mdogo wa Mirerani, mkoani Manyara jana. Kulia ni Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Madini nchini (FEMATA), John Bina. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

## Waliosamehewa na Magufuli Arusha waondolewa

UKURASA 3

### BAA LA CORONA



Watu wanaweza kupata maambukizi ya virusi vya corona kwa kushika sehemu na vitu ambavyo vimedondokewa na majimaji yenye virusi hivyo na baadaye kugusa macho, pua au mdomo. Ndio maana inashauriwa kuosha mikono kwa sabuni mara kwa mara. WHO

* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

**MICHEZO** **YANGA, MORRISON FILAMU INAENDELEA** UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Mchimbaji mdogo alamba bilioni 7/-

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

SERIKALI imemkabidhi hundi ya Sh. bilioni 7.7, mchimbaji mdogo wa madini ya Tanzanite, Saniniu Laizer, baada ya kununua mawe mawili yenye uzito wa kilogramu 14.

Kati ya mawe hayo, moja lililoweka rekodi ya ukubwa katika historia ya uchimbaji wa madini hayo yanayopatikana Tanzania pekee, ni la kilogramu tisa.

Vito hivyo vya thamani kuwahi kupatikana nchini, vilivumbuliwa na mchimbaji huyo katika eneo la Kitalu D kilichoko Mirerani, Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara.

Wakati wa hafla ya kutia saini ununuzi wa madini hayo kati ya serikali na mchimbaji huyo jana wilayani huko, ilielezwa kuwa mawe hayo yatahifadhiwa kwenye Makumbusho ya Taifa, ili kuvutia watalii kujionea fahari ya Tanzania.

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano ya mawe hayo kwenye eneo la Mirerani, Waziri wa Madini, Doto Biteko, alimpongeza mchimbaji huyo kwa kuwa mzalendo na kukubali kuiuzia serikali bila kipingamizi.

Alisema kitendo cha mchimbaji mdogo kupata mawe hayo kumeidhihirishia ulimwengu kuwa wachimbaji wadogo wanaweza na hasa wakiwezeshwa.

"Tunachoagiza, mchimbaji huyu asidhuriwe na yeyote na ruksa fedha hizo kuwekeza kwa chochote atakachotaka kwani ni zake," Biteko alisema.

Alibainisha kuwa mara tu baada ya kupatikana madini hayo, Rais John Magufuli aliagiza serikali kuyanunua, ili yawekwe kwenye makumbusho kwa ajili ya kuidhihirishia dunia kuwa Tanzania ndiyo kitovu cha madini.

"Endapo tungeuzia nchi zingine, sisi tungefunga safari kwenda kuona wakati yametoka kwetu, hilo haliwezekani," alisema.

Waziri huyo alisema Rais Magufuli pia anastahili pongezi kwa kuwa tangu ajenge ukuta kuzunguka eneo lote la mgodi Septemba 2017, kumekuwa na ongezeko la mapato ya madini kutoka Sh. bilioni 470 hadi Sh. bilioni 526 kwa mwaka.

Alisema katika makusanyo hayo, sehemu kubwa inatoka kwa wachimbaji wadogo ambao wanalipa mrabaha wao serikalini.

"Ninaomba tuwalee na kuwashika mkono wachimbaji hawa badala ya kuendelea na maneno ya kejeli kwao kuwa hawana teknolojia na mitaji ya kuchimba madini hayo," alisema.

Kuhusu kuwapa wachimbaji wadogo kitalu C kilichokuwa kinamilikiwa na mwekezaji Tanzanite One kwa ubia na serikali, Biteko alisema wanaweka utaratibu ili wawape wachimbaji hao.

Kwa mujibu wa Biteko, tayari uongozi wa Mkoa wa Manyara umeshaagizwa kulinda Kitalu C ambacho sasa ni mali ya serikali baada ya kukifunga ili kisivamiwe na yeyote.

**JPM APIGA SIMU**

Wakati hafla hiyo ikiendelea huku ikirushwa moja kwa moja na Televisheni ya Taifa (TBC), Rais Magufuli alimpigia simu Waziri Biteko na kuwapongeza wachimbaji wadogo waliohudhuria hafla hiyo.

Kiongozi huyo wa nchi pia alimpongeza Laizer na kueleza kuwa hiyo ndiyo faida ya wachimbaji wadogo wadogo.

"Hii ni kudhihirisha kwamba Tanzania sisi ni matajiri, ninakupongeza Waziri wa Madini, Wizara ya Fedha, Gavana (wa Benki Kuu), viongozi Mkoa wa Manyara, Kilimanjaro na Arusha na ninawapongeza sana wananchi wa Simanjiro kwa shughuli wanazozifanya katika kujitajirisha.

"Tanzanite hii ni kubwa sana, haijawahi kupatikana mahali pengine ndiyo maana ninamshukuru Gavana, Waziri wa Fedha chini ya uongozi wako, waziri kwa kuamua kuinunua nilikuwa ninaangalia hapa, nimefurahi kuwaona, Mungu awabariki sana," alisifu.

Rais Magufuli alimpongeza Laizer na kumtania kuwa anaamini anakwenda kuongeza mke, akimshauri akatafute mke kutoka kabila la Wasukuma.

Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo, pia alimpongeza mchimbaji huyo kwa kuwa mwaminifu kwa kuwa katika kipindi cha 2019/20, amechimba madini ya kilo 108 na serikali ikapata mrabaha wa Sh. milioni 638.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Ashatu Kijaji, alisema serikali imenunua madini hayo kwa zaidi ya Sh. bilioni 7.7 na amekabidhiwa fedha zake akafanye atakachoona kinafaa.

"Hizi fedha ni za walipa kodi, tunaomba endeleeni kulipa kodi ili tufanye makuu zaidi na kuwezeshana wenyewe," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, alisema kupatikana kwa madini hayo ni matunda ya kujenga ukuta kuzunguka eneo la Mirerani.

"Kabla ya ukuta huu, tulikuwa tunapata madini haya kilo 300 yenye thamani ya Sh. bilioni nne kwa mwaka, ila tangu ujengwe ukuta huu, tunapata madini zaidi ya kilogramu 4,000 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 50, kweli tunamshukuru Rais John Magufuli," alisema.

Aliiomba serikali igawe kwa wachimbaji wadogo Kitalu C ambacho kimekuwa mali ya serikali na kinazalisha zaidi madini hayo, baada ya kukitaifisha, ili wazalishe zaidi madini hayo na kulipa kodi kwa serikali.

Mbunge wa Simanjiro, James Millya, pia aliomba kitalu hicho wapewe wachimbaji wadogo na kuwasaidia zana za uchimbaji, ili wachimbe kisasa zaidi.

"Tunasema wapewe hawa wadogo kwa sababu hata mawe haya ya mabilioni yaliopatikana, yamepatikana kwa mchimbaji mdogo, hivyo wanaweza," alisema.

Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji wa Madini nchini, John Bina, alisema wataleta mapinduzi zaidi kwenye madini hayo kwa kupata mawe makubwa zaidi ya hayo.

"Tumpe zawadi Rais Magufuli, tumpe zawadi apite bila kupingwa ili wakati wa uchaguzi aangalie wabunge wakimenyana jimboni, maana bila yeye yasingepatikana madini hayo," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wa Madini, (TAMIDA), Sam Mollel, alisema kitendo cha mchimbaji mdogo kuvumbua madini hayo imedhihirisha wachimbaji wadogo wanaweza kufanya maajabu zaidi.

Laizer kwa upande wake, aliishukuru serikali kwa kuyanunua madini hayo na kuahidi kuwa atawekeza kwenye elimu na kujenga miradi mbalimbali ya kiuchumi.

# Lowassa, mkewe wamdhamini JPM

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI Mkuu wa zamani, Edward Lowassa na mke wake, Regina Lowassa, wameungana na mamia ya wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Arusha kumdhamini mgombea urais kwa tiketi ya chama hicho, Rais John Magufuli.

Rais Magufuli anatarajiwa kutetea nafasi yake katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu akiwa hajapata upinzani ndani ya chama chake mpaka sasa.

Hatua ya Rais Magufuli kutopata mpinzani ndani ya chama chake kunatokana na utaratibu uliowekwa ndani ya CCM wa kumwachia Rais aliyeko madarakani amalizie kipindi chake cha pili cha miaka mitano.

Jana, Lowassa na mamia ya wanachama wa chama hicho walikusanyika kwenye Ofisi ya CCM Wilaya ya Monduli kutia saini zao kwa ajili ya kumdhamini mgombea huyo wa urais, ili kukidhi matakwa ya katiba ya chama hicho.

Katiba ya CCM inamtaka kila anayetaka kugombea urais kwa tiketi ya chama hicho, kudhaminiwa na wanachama 450 kwa mikoa minane ya Bara na miwili ya Zanzibar.

Lowassa ni mwanasiasa machachari ambaye baada ya jina lake kukatwa na Kamati Kuu iliyoongozwa na Mwenyekiti wa CCM wakati huo, Dk. Jakaya Kikwete, alihamia Chadema na kusimamishwa kuwania urais kwa tiketi ya vyama vinavyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa) katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.



Waziri Mkuu mstaafu na Mbunge wa zamani wa Monduli, Edward Lowassa, akijaza fomu ya kumdhamini mgombea urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli, ili atetee kiti chake katika uchaguzi mkuu ujao wa Oktoba mwaka huu, wilayani Monduli, mkoani Arusha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Akiwa mgombea wa Ukawa, Lowassa atakumbukwa kwa namna alivyotia hamasa uchaguzi huo, akichuana vikali na aliyekuwa mgombea urais wa CCM, Rais Magufuli na kufanikiwa kupata kura milioni 6,072,848 dhidi ya milioni 8.882,935 za mshindi.

Katika vuguvugu la uchaguzi huo wa mwaka 2015 ndani ya CCM, jina la Lowassa lilionekana kuwa maarufu kati ya wagombea wengine 42 waliojitokeza kukiomba chama chao kupeperusha bendera yake kwenye uchaguzi huo.

Na kwenye hatua za awali ambapo CCM ilimtaka kila mgombea kudhaminiwa na angalau wanachama 450, Lowassa alifikisha watu 700,000 waliokubali kumdhamini, ingawa jina lake lilikatwa katika hatua za mwanzo kabisa na kukosekana katika yale yaliyoingia hatua ya tano bora.

Katika mchakato huo baadhi ya wajumbe wa Kamati Kuu (CC) ya CCM walitoka hadharani na kutamka mbele ya waandishi wa habari kuwa hawakubaliani na uamuzi wa kumkata Lowassa.

Wajumbe wa CC, Adam Kimbisa, Dk. Emmanuel Nchimbi na Sophia Simba, aliyekuwa Mwenyekiti wa UWT, walisema kuna njama zilifanyika na walisema waziwazi kwamba hawakubaliani na uamuzi huo wa CC.

NEC ilipokaa kupokea majina yaliyopitishwa na CC kwa ajili ya kupigiwa kura, baadhi ya wajumbe walisimama na kuimba kuwa wana imani na Lowassa wakati Mwenyekiti wa chama hicho wakati huo, Dk. Kikwete alipokuwa akiingia ukumbini.

Baada ya mchakato huo wa kumpata mgombea wa CCM, Lowassa aliamua kuhamia Chadema akifuatwa na kundi kubwa la wana CCM kukihama chama hicho wakiwamo waliokuwa na nyadhifa mbalimbali kama wabunge, wenyeviti wa mikoa na makatibu.

Machi Mosi, mwaka jana, Lowassa alitangaza kurejea CCM na kupokelewa na Mwenyekiti wa chama hicho, Rais Magufuli kwenye ofisi ndogo za chama hicho jijini Dar es Salaam.

Katika maelezo mafupi aliyoyatoa mbele ya wafuasi wachache wa CCM walioshuhudia kurejea kwake siku hiyo, Lowassa alisema kwa kifupi "nimerejea nyumbani".

KILICHOMPAISHA

Kilichompaisha zaidi Lowassa katika hekaheka zake za kisiasa ni kambi yake ya urais iliyobatizwa jina la utani 'Boys Two Men' mwaka 1995.

Ni kambi iliyowahusisha Dk. Kikwete na Lowassa ambapo mwaka 1995 walikwenda Dodoma kwa ndege ya kukodi kuchukua fomu za kuomba ridhaa ya kuteuliwa kugombea urais kwa tiketi ya CCM.

Safari ya wawili hao ilianza kufifia baada ya jina la Lowassa kukatwa mapema na jina la Kikwete kufika kwenye mkutano mkuu uliofanyika Ukumbi wa Chimwaga mkoani Dodoma.

Matumaini ya Boys Two Men yalibaki kwa Kikwete lakini mkutano mkuu wa CCM uliohudhuriwa na Mwalimu Nyerere ulikatisha ndoto ya Kikwete baada ya Benjamin Mkapa kuteuliwa kuwa mgombea urais kupitia CCM katika Uchaguzi Mkuu wa 1995.

Wakati Kikwete anamalizia awamu yake ya pili, Lowassa alikuwa bado na imani ya ushirikiano wa Boys Two Men, lakini mambo hayakuwa hivyo kwani jina lake lilikatwa kwenye Kamati ya Maadili ya CCM na baadaye alilazimika kutimkia Chadema.

Lowassa aliyezaliwa Agosti 26, 1953 huko Monduli mkoani Arusha, aliteuliwa na Kikwete kuwa Waziri Mkuu hadi Februari 2008 alipojiuzulu kwa kashfa ya kampuni tata ya Richmond. fanyika kwake kuna taratibu zake ambazo lazima zifuatwe.

# Waliosamehewa na JPM Arusha waondolewa nafasi zao

**Na Romana Mallya**

KAMANDA wa Polisi wa Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana na Mkuu wa TAKUKURU mkoani humo, Frida Wikes, ambao Rais John Magufuli alitangaza kuwasamehe, wameondolewa kwenye nafasi hizo.

Jumatatu, Rais Magufuli wakati akiwaapisha viongozi aliowateua Ikulu jijini Dar es Salaam, alitangaza kuwasamehe viongozi hao ambao walikuwa wakifanya kazi ambazo hajawatuma.

Taarifa za kuondolewa kwao zilisambaa jana kwenye mitandao ya kijamii ambapo Nipashe ilizithibitisha kupitia mamlaka wanazozifanyia kazi ambazo zilikiri ni za kweli.

Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, (IGP), Simon Sirro, aliliambia gazeti hili kuwa, ni kweli Jeshi la Polisi limemuondoa Kamanda Shana na kumwamishia Chuo cha Polisi Moshi, mkoani Kilimanjaro.

"Ni kweli ameondolewa, hayo ni mabadiliko ya kawaida ndani ya Jeshi la Polisi, tuliona kuna upungufu pale chuoni tukampeleka kuongeza nguvu, ameondolewa leo (jana)," alisema.

Wakati huo huo, Sirro amefanya uhamisho kwa baadhi ya Makamanda wa Polisi wa mikoa ili kuongeza ufanisi na tija katika kazi za Polisi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, SACP David Misime, awaliohamishwa ni Kamanda wa Polisi mkoa wa Kilimanjaro, ACP Salum Hamdunim kwenda kuwa Kamanda wa Polisi mkoa wa Arusha.

Kuchukua nafasi ya Shana. Pia, IGP Sirro, amemhamisha aliyekuwa Afisa Mnadhimu Bunge, Dodoma ACP Emmanuel Lukula, kwenda kuwa kamanda wa Polisi mkoa wa Kilimanjaro na nafasi yake inachukuliwa na ACP Andrew Satta ambaye alikuwa Afisa Mnadhimu Makao Makuu ya Polisi Dodoma.

Naye, Ofisa Uhusiano wa TAKUKURU, Doreen Kapwani, alikiri taasisi hiyo imemuondoa Wikes na kumwamishia Makao Makuu. Akizungumza siku hiyo, Rais Magufuli alisema: "Leo nilikuwa niwatoe RPC (Kamanda wa Polisi) pamoja na Mkuu wa TAKUKURU, Arusha nimeona niwaonye hapa hapa, nimeamua kuwasamehe, lakini sijawasamehe moja kwa moja wakifanya kosa lolote wataondoka.

"Ninataka wakafanye kazi nilizowatuma siyo kazi wanazojituma wao, ninajua mtawafikishia salamu nimejitahidi sana kuwasamehe."

Alisema haiwezekani ukawa umewatuma watu wakafanye kazi za serikali wanafanya shughuli zao.

# Maiti za vichanga zapotea kiajabu hospitali ya mkoa

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MKUU wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, ametoa siku saba kwa Jeshi la Polisi kuhakikisha linawafikisha mahakamani watumishi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa huo waliosababisha kupotea kwa maiti mbili za watoto wachanga.

Homera alitoa agizo hilo jana, akisisitiza kuwa ni uzembe maiti kupotea ilhali wasimamizi wa chumba cha kuhifadhi maiti katika hospitali hiyo wapo.

Alisema watumishi katika chumba hicho wanapaswa kusimamishwa kazi mara moja ili kupisha uchunguzi unaoendelea.

Kiongozi huyo wa mkoa alisema hakuna haja kuendelea kukaa na watumishi wanaosababisha shida katika idara, akihoji sababu za kupotea kwa maiti hizo na watumishi hao kutokujua zilikopelekwa ilhali wameajiriwa ili kuhakikisha hakujitokezi matatizo katika idara hiyo. Hata hivyo, Homera alilihusisha tukio hilo na imani za kishirikina, akiwataka wanasiasa na wadau wa madini kutojihusisha na vitendo hivyo.

"Hatuwezi kusubiri mtu mwingine aje atatue matatizo ya Katavi wakati kuna mkuu wa mkoa, wakuu wa wilaya na viongozi wengine. Inaonekana kuna watu wanadanganywa, ukifanya hivyo utashinda uchaguzi, au utapata madini mengi, na huu mchezo unaonekana ulikuwapo," alisema.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa huo, Dk. Justina Tizeba, alidai kuwa siku ya tukio, alipokea taarifa kutoka kwa muuguzi mfawidhi zikimtaka afike hospitalini huko kwa kuwa kulikuwa na tatizo la kupotea kwa maiti mbili za watoto wachanga.

Alisema kuwa baada ya kufika hospitalini, waliwahoji watendaji katika chumba cha kuhifadhi maiti ambao walikiri kupokea maiti hizo na kuzihifadhi, lakini zilizotakiwa kutoka, hazikuonekana na hawakujua zilikokwenda.

Dk. Tizeba alisema kuwa walitoa taarifa kituo cha polisi na wahusika walikamatwa na kuwekwa mahabusi, lakini baadaye waliachiwa kwa dhamana.

Rebecca Faustine, mmoja wa wazazi wa walipoteza watoto hao muda mfupi baada ya kujifungua, alisema aliumwa uchungu Jumamosi na alipojifungua, hakujua alikopelekwa mtoto wake.

"Baadaye wifi yangu na mume wangu ilibidi wamuulize nesi 'mtoto yuko wapi?' Na nesi alijibu kuwa mtoto alifariki dunia, lakini walipoomba maiti wakazike, maiti haikuonekana hadi sasa," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, akipokea zawadi ya kuku na mafuta ya kupikia kutoka kikundi cha Upendo, alipotembelea vikundi wezeshi ikiwa ni sehemu ya uhamasishaji na utekelezaji wa Mradi wa Hebu Tuyajenge, unaotekelezwa na Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na VVU (NACOPHA), kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Watu wa Marekani USAID wilayani Sikonge, mkoani Tabora juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake wengine 2 wajitosa urais, kada NCCR-Mageuzi naye atangaza nia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IDADI ya wanawake wanaotaka kumrithi Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, imeongezeka baada ya jana makada wawili kujitokeza kuchukua fomu ya kugombea urais wa Zanzibar.

Tangu uchukuaji fomu uanze Juni 15, makada 25 wa CCM wameshachukua fomu na kati ya hao watatu ni wanawake.

Jana majira ya saa 4:00 asubuhi, Hasna Attai Masoud, ambaye ni mtumishi wa Serikali ya Zanzibar alifika ofisi kuu za CCM kuchukua fomu hiyo na majira ya 7:00 mchana mwanamama mwingine, Fatma Kombo Masoud, mjasiriamali alichukua fomu hiyo.

Wanawake hao walisema kuwa kazi iliyo mbele yao hivi sasa ni kutafuta wadhamini 250 ili kurejesha fomu hiyo.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Idara ya Oganizesheni ya CCM, Galous Nyimbo, alisema chama hicho akina ubaguzi, hivyo nafasi hiyo inaweza kugombewa na kada yeyote.

Alisema wanawake hawapo nyuma kuwania nafasi za uongozi na ndio maana wamethubutu kugombea nafasi ya urais.

"Leo zoezi la uchukuaji fomu limetawaliwa na wanawake maana hadi muda huu waliochukua fomu ni wanawake tu, nawapongeza wanawake kwa ujasiri wao," alisema.

Alisema makada sita tayari wamesharudisha fomu baada ya kukamilisha masharti ikiwamo kupata wagombea 250 kutoka mikoa mitatu ya Zanzibar.

"Waliorejesha fomu ni Mbwana Bakari Juma, Balozi Ali Karume, Balozi Muhammed Hija, Dk. Abdulhalim Muhamed, Dk. Hussein Mwinyi na wametimiza masharti," alisema.

Akizungumza baada ya kurudisha fomu hizo, Waziri wa Ulinzi, Dk. Hussein Mwinyi, alisema ameshakamilisha masharti, anachosubiri sasa ni uamuzi wa chama.

Alisema CCM ni chama chenye demokrasia na ndio maana idadi ya waliochukua fomu imefikia 25, hivyo vikao vya chama ndio vitakavyoamua mgombea yupi atakayepitishwa.

Watia nia waliochukua fomu hadi jana ni Mbwana Bakari, Balozi Ali Karume, Mbwana Mwinyi Yahya, Omar Shehe, Muhammed Jafar, Muhammed Hija, Meja Jenerali Issa Suleiman Nassor, Shamsi Vuai Nahodha, Dk. Hussein Mwinyi, Profesa Makame Mbarawa, Mwatum Mussa Sultan, Haji Rashid Pandu na Dk. Abdul-halim Mohammed Ali, Jecha Salim Jecha na Dk. Khalid Salum Muhamed.

Wengine ni Rashid Ali Juma, Khamis Mussa, Mmanga Mjengo Mjawiri, Hamad Yussuf Masauni, Muhammed Aboud, Bakari Rahid, Ibrahim Makungu, Ayoub Muhammed Mahmoud, Hashim Salum Hashim, Hasna Ataai Maoud na Fatma Kombo Masoud.

# Polisi wavamia mkutano wa THRDC, wahoji wawili

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi mkoa wa kipolisi wa Kinondoni, jana lilizuia kufanyika mkutano wa watetezi wa haki za binadamu kwa kile walichodai ni kutoridhishwa na maudhui yake.

Tukio hilo lilitokea jana jijini Dar es Salaam, wakati watetezi hao 33 kutoka kanda 11 nchini wanajiandaa na mkutano huo, walifika polisi na kuwakamata wawezeshaji wawili.

Mkutano huo ulipangwa ufanyike kwa siku tatu katika jengo la Millenium Tower Makumbusho Jiji Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mratibu wa Mtandao huo nchini, Onesmo Olengurumwa, alisema polisi walifika asubuhi kwenye ukumbi huo na kuwachukua wawezeshaji hao na kuwapeleka kituoni.

"Tunasikitika sana hadi sasa tunashindwa kuanza mafunzo yetu kutokana na kwamba polisi walivamia na kuchukua baadhi ya wafanyakazi wa THRDC wawili waliokuwa wanashughulika na mafunzo haya," alisema.

"Mikutano ya ndani ni shughuli za kawaida za asasi za kiraia, na tumeshangazwa sana kuona polisi wanaingilia shughuli zetu za ndani... tunaomba wale waliowatuma askari hao kuacha mara moja kuingilia shughuli za ndani za asasi za kiraia," alisisitiza.

Alisema polisi hao mara ya kwanza waliwaeleza kuwa hawaruhusiwi kukusanyika kwa sababu ya janga la corona, na kwamba inashangaza kwa kuwa Rais alisharuhusu wananchi kuendelea na shughuli zao kama kawaida.

"Tunashangazwa na zuio hili, tulikua tualike wanachama wetu 55 nchini, lakini kutokana na corona na kwa kuzingatia umbali wa mtu na mtu, tumealika watu 33," alifafanua.

Kwa mujibu wa Olengurumwa, wamfuatilia suala hilo kwa RPC (Kamanda wa Polisi) wa Kinondoni, lakini hawajapewa jibu kamili.

"Tumeshawaleta watu kutoka mikoani kwa siku tatu na sasa polisi wanasema haturuhusiwi kufanya mkutano, awali walisema kwa sababu ya corona na sasa wanasema hatukutoa taarifa za mkutano kueleza tunawafundisha nini watu, na kwamba tunafundisha masuala ya usalama ambayo ni jukumu la polisi kutoa elimu hiyo," alibainisha Olengurumwa.

Akizungumzia tukio hilo, Kamanda wa Polisi Kinondoni, Mussa Taibu, alithibitisha kukamatwa kwa wafanyakazi hao, na kwamba lengo ni kuweka sawa maudhui yaliyokuwa yaongelewe kwenye mkutano huo.

"Tuliwachukua viongozi hao kwa ajili ya mazungumzo kujiridhisha na maudhui ya mkutano huo, hakuna aliyekamatwa,lengo letu ni kujua maudhui yatakayozungumzwa," alifafanua Kamanda Taibu.

***Imeandikwa na Mary Mshami, Magdalena Haule na Fatma Mtutuma (UDOM)***




Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, akifungua mafunzo kwa watetezi wapya kuhusu jinsi ya kufanya kazi bila kuvunja sheria za nchi, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Programu Meneja wa mtandao huo, Remmy Lema na Ofisa Uwezeshaji, Catherine Ringo. **PICHA: MIRAJI MSALA .**

## REA yatishia kuzuia hati ya mkandarasi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAKALA wa Umeme Vijijini (REA), umetishia kuzuia hati za kusafiria za makandarasi wa umeme wa Kampuni ya A2Z Infra Ltd hadi watakapokamilisha utekelezaji mradi wa REA III awamu ya kwanza, jijini Dodoma.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala huo, Henry Mwalwinza, alisema kampuni hiyo inapaswa kukamilisha mradi huo Juni 30, mwaka huu, lakini hadi sasa utekelezaji upo asilimia 61.

"Bado asilimia 39 ya mradi haijatekelezwa hatutakuwa tayari kuwaongezea muda mrefu kinachotakiwa ni wakamilishe ujenzi huu, kinyume cha hapo tutazuia hati zao za kusafiria,"alisema.

Alisema serikali inahitaji kuona wananchi wake wanakuwa na umeme.

Alisema,endapo watashindwa kutekeleza mradi huo kwa wakati, Bodi itawasilisha taarifa na kuikabidhi kwa Mamlaka husika kwa hatua zaidi ikiwamo kuwanyang'anya hati za kusafiria wasiondoke nchini.

"Hatutaongeza muda na wala hatuna masihara katika eneo hilo, tunawatakia kukamilisha kazi ya kusambaza umeme vijijini kwa mkoa wa Dodoma kwa mujibu wa mkataba, na wakishindwa tutawasiliana taarifa hiyo kwa mamlaka husika kwa hatua zaidi," alisema.

Naye, Meneja wa kampuni hiyo, Yazir Azmi, aliomba waongezewe muda wa miezi miwili ili wakamilishe shughuli utekelezaji wa mradi huo.

"Bado kuna kipande kirefu ambacho kinahitaji muda kidogo ili ukamilike utekelezaji mradi huu, na sababu zilizofanya tuchelewe ni mvua zilizonyesha mfululizo,"alisema.

Alisisitiza kuwa mradi huo lazima ukamilike ili wapewe miradi mingine ya kutekeleza bila kuwa na mgogoro.

# LATRA yaja na leseni mpya kwa madereva mtandaoni

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imeanza kutoza ada za leseni kwa madereva mtandaoni na kutaka kila mmoja kukata leseni hiyo kabla ya Agosti, mwaka huu.

Aidha, madereva wa magari hayo wamelalamikia utitiri wa kodi kwa kila mamlaka, huku wamiliki wa mitandao hiyo wakiwatoza fedha nyingi kwa kila safari.

Kwa mujibu wa tangazo la LATRA, kila dereva anapaswa kulipa ada ya mwaka ya maombi ya Sh. 10,000 na gharama za leseni ya Sh. 25,000.

Ili ufanye biashara ya kuendesha magari mtandaoni ni lazima ulipe Sh. 80,000 kupata leseni ya jiji, Sh. 25,000 kupata leseni ya manispaa, kodi ya TRA ambayo huanzia Sh. 250,000 hadi 350,000.

kwa mujibu wa taarifa iliyotumwa kwa madereva wa mtandao wa Uber, ikiwa na kichwa cha habari 'Mwongozo mpya stika za LATRA', ni lazima kuwa na kibali hicho ndiyo utaruhusiwa kufanyakazi kuanzia Julai mosi, mwaka huu.

"Kutokana na mabadiliko yaliyofanyika hivi karibuni, unahitajika kuwa na stika ya LATRA ili kufanyakazi katika mfumo wowote wa usafirishaji," alisema na kuongeza:

"Uber imetoa stika ya jiji kwa Uberx na Uberxl pamoja na SUMATRA kwa Uberpoa kama nyaraka zinazohitajika ili kufanya kazi. Itaweka ya LATRA badala ya hizo zilizotajwa."

Pia, ujumbe huo unawataka madereva kuomba leseni hiyo mtandaoni kwenye tovuti ya LATRA na kuambatanisha kadi ya usajili wa gari, hati ya biashara, hati ya ukaguzi wa gari kutoka Jeshi la Polisi na leseni ya udereva.

"LATRA itaanza kutia mkazo kwa magari yasiyokuwa na leseni kuanzia Agosti, kisheria unatakiwa (dereva) kuwa na leseni hiyo, ikifika hiyo tarehe kwa madereva wa zamani, lakini kwa wapya ni lazima wawe na stika hiyo kabla ya kusajiliwa," ulifafanua ujumbe huo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, LATRA haijatoa taarifa zozote kuhusu wakala atayekusanya fedha hizo na madereva wanatakiwa kutuma maombi mtandaoni na kusubiri majibu kwenye barua pepe zao.

Akizungumza leseni hizo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Gilliard Ngewe, alisema jambo hilo ni utekelezaji wa kanuni za sheria zilizotangazwa Februari mwaka huu.

HABARI KITAIFA

# Mpango mkakati wa DCB miaka mitano kujadiliwa

**Na Mwandishi Wetu**

WANAHISA wa BENKI ya Biashara ya DCB wanatarajia kujadili mpango mkakati wa benki hiyo wakati wa mkutano mkuu wa mwaka unaotarajiwa kufanyika Jumamosi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa DCB, Godfrey Ndalahwa, alisema, mkutano huo utakuwa wa kihistoria kwani ni kwa mara ya kwanza utafanyika kwa njia ya mtandao.

Akizungumzia mafanikio ya mkakati wa miaka mitano ya utendaji wa DCB, alisema wanahisa watajadili ajenda mbili ambazo ni kuelezwa gawio la mwaka, lakini kujua taarifa ya tathmini ya mkakati wa miaka mitano uliojiwekea.

"Ikumbukwe kuwa mwaka 2017, uongozi na Bodi ya Wakurugenzi iliandaa na kupitisha mpango mkakati wa miaka mitano (2018-2022) ambao ulilenga kuirejesha benki katika mstari kutoka kwenye hasara hadi faida, kuiimarisha benki ili kuiweka sawa na tayari kwa ukuaji endelevu na upanuzi," alisema Ndalahwa na kuongeza:

"Kufikia mwisho wa mwaka 2018, benki ilikuwa imekamilisha awamu ya kwanza ya mpango huo baada ya kupata faida ya Sh. bilioni 1.6 .

"Wakati tunafunga mwaka 2019, benki ilikuwa imekamilisha hatua ya pili ya mpango mkakati huo ikiwa ni uimarishaji kupitia mafanikio ya zoezi la uuzaji wa hisa stahiki kwa wanahisa na kupata Sh. bilioni 9.7 kutoka kwenye lengo la Sh. bilioni 8.9, ikiongeza mtaji wa hisa kutoka Sh. bilioni 16 mwaka 2018 hadi bilioni 25 mwaka 2019. Hisa hizi mpya zilizorodheshwa na sasa zinaendelea kuuzwa katika soko la hisa."

Alisema kazi kubwa imefanyika katika kurudisha benki kwenye faida, ambapo kwa mwaka 2019 ulikuwa mwaka mwingine wa mafanikio makubwa, ambapo waliweza kupata faida kabla ya kodi ya Sh. bilioni 2.10. Alisema ongezeko la asilimia 30 ikilinganishwa na 2018 ambapo faida ilikuwa Sh. bilioni 1.62.

Kwa mujibu wa Ndalahwa, uendelezo wa faida ulichochewa na ukuaji wa mizania na uboreshaji ufanisi wa kiutendaji. Jitihada hizi zilisababisha ukuaji wa asilimia 14 katika amana za wateja, ukuaji wa asilimia 11 kwa mikopo ya wateja, ukuaji wa asilimia 22 katika mapato yasiyofadhiliwa na asilimia 9 kupungua kwa gharama za uendeshaji.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya DCB, Godfery Ndalahwa (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mkutano mkuu wa wanahisa wa benki hiyo, unaotarajiwa kufanyika Juni 27 kwa njia ya video, ambapo wanahisa 7,000 watashiriki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgodi watoa kadi za afya kwa wazee 450

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

WAZEE 450 wanaozunguka mgodi wa madini ya dhahabu wa Barrick-Bulyanhulu, wilayani Kahama, wamepewa kadi za matibabu bure kwa ajili ya kuboresha afya zao.

Akizungumza jana wakati wa kukabidhi kadi hizo, Kaimu Meneja Maendeleo ya Jamii kutoka mgodi huo, Zuwena Senkondo, alisema mgodi huo hutenga fedha kwa ajili ya kuhudumia makundi maalumu yanayozunguka mgodi.

Alisema mwaka jana walitenga Sh. milioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa jamii na asilimia 10 kusaidia makundi maalumu.

"Mgodi wetu wa Bulyanhulu kila mwaka tunatenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa maendeleo ya jamii inayotuzunguka, pamoja na kuhudumia makundi maalumu wakiwamo wazee na wenye ulemavu kwa kuwapatia vifaa wezeshi na kadi za matibabu bure," alisema Senkondo. "Tumetoa kadi 450 za matibabu bure kwa wazee wanaozunguka mgodi wetu kutoka kata ya Bugharama na Bulyanhulu, ili kuwarahisishia upataji wa matibabu na kuboresha afya zao, na zoezi hili litakuwa endelevu," aliongeza.

Alisema pia wametoa baiskeli nane kwa watu wenye ulemavu, fimbo nyeupe tano, pamoja na magongo matano, vitu vyote vikigharimu Sh. milioni 8.05.

Baadhi ya wazee waliopatiwa kadi hizo Iddi Bingi, waliushukuru mgodi huo kwa kuwajali wazee na kuomba kuboresha zaidi huduma za afya maeneo ya vijijini pamoja na upatikanaji wa dawa kwa wazee.

Kwa upande wa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, aliwatoa wasiwasi wazee hao kuhusu uhaba wa dawa na kuwa serikali imeshaagiza kila zahanati na vituo vya afya, vihakikishe dawa za wazee zinakuwapo pamoja na utengaji wa madirisha ya mpishe mzee kwanza.

# Kairuki avutiwa uwekezaji kiwanda cha kuku, mboga

**Na Mwandishi Wetu, IRINGA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, amevutiwa na uzalishaji wa chakula cha kuku, ufugaji wa kuku pamoja na mboga katika Kongani ya Ihemi kwenye ushoroba wa Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT).

Amesema uwekezaji huo unakwenda sambamba na azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Nimevutiwa sana na uwekezaji huu wa kiwanda cha kutengeneza chakula cha kuku, ufugaji wa kuku na kilimo cha mboga. Serikali tutaendelea kuboresha na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji nchini," alisema Waziri Kairuki.

Akizungumza kwa nyakati tofauti jana alipotembelea kiwanda cha ufugaji na uzalishaji wa chakula cha kuku cha Silverlands, Masifio Sstates, Pyrethrum Tanzania (PCT), Qwihaya General Entreprises na Sao Hill, Waziri Kairuki alisema uwekezaji wa kuku na kilimo cha mboga katika eneo hilo una mchango mkubwa katika kuongeza kipato kwa wakazi wa Iringa.

" Hii siyo hadithi, nimejionea mwenyewe namna uzalishaji mkubwa wa kuku na mboga unavyofanyika, na sisi kama serikali tutahakikisha tunawaunga mkono ili kujenga na kuimarisha sekta hasika pamoja kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi nchini," alisema.

Alisema kiwanda cha Silverlands kimekuwa chachu ya maendeleo kwa upande wa kuku, lakini pia wamekuwa wanunuzi wakubwa wa zao la mahindi kutoka kwa wakulima wa mikoa ya nyanda za juu kusini na hivyo kuliongezea thamani zao hilo.

Waziri Kairuki alionyesha pia kufurahishwa na kilimo cha mboga katika shamba la Sasifio, akisema kimetoa mchango mkubwa wa kukidhi mahitaji ya mahoteli pamoja na sekta ya utalii kwa kuzalisha aina 14 za mboga ambazo nyingi awali zilikuwa zikiagizwa kutoka nje ya nchi.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, alikipongeza kiwanda cha Silver Lands kwa mchango wake katika maendeleo ya mkoa kwa kuwahakikishia wakulima soko la uhakika la mazao ya mahindi na soya.

Naye mwekezaji katika shamba la Masifio, Quitin Robb alikipongeza Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuhakikisha mazingira ya uwekezaji yanakuwa rafiki.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Uwepo ufumbuzi endelevu usafirishaji wa wanafunzi*

WIKI ijayo shule zinafunguliwa rasmi na suala la usafiri kwa wanafunzi mijini na kwenye majiji linahitaji jicho la tatu kwa kuwa ni changamoto isiyo na jibu wala ufumbuzi endelevu.

Kuna haja ya kulitizama suala hilo kwa umakini kwa vile shule zote za msingi na sekondari zitakapofunguliwa zitaongeza idadi ya wanafunzi barabarani na kwenye vituo vya mabasi.

Ni muhimu kuchukua hatua sasa kwa sababu watoto wengi wanatumia usafiri wa magari ya umma ili kufika shuleni na kurudi nyumbani.

Kutokana na kuwapo kwa corona utaratibu wa abiria ni kukaa kwenye gari kulingana na idadi ya viti jambo ambalo limeleta changamoto kwa abiria kukaa muda mwingi vituoni na hata kulazimika kuunganisha daladala zaidi ya moja.

Katika mwonekano huo, hiyo ni changamoto kwa wasafiri wa kawaida wa mijini na kwenye majiji. Ni wazi kuwa kama utaratibu huo utaendelea kuzingatiwa wanafunzi watateseka licha ya kwamba mkoani Dar es Salaam, daladala zimeruhusiwa kuwapa wanafunzi watano nafasi za kusimama.

Inavyoelekea kwa utaratibu wa sasa wanafunzi watapata changamoto ya kupata usafiri kwa wakati hivyo ni vyema kabla ya kufungua shule kuwepo na maelekezo.

Licha ya kwamba hata kabla ya shule kufungwa mabasi yaendayo haraka au mwendokasi yalikuwa yanawabeba wanafunzi wengi, kuwapo kwa ugonjwa wa corona na kupunguza idadi ya abiria ni tatizo, ambalo linaelekea kukwamisha mabasi hayo kubeba wanafunzi wengi zaidi.

Kwa Dar es Salaam, serikali imetoa kibali maalumu kwa magari binafsi kupeleka abiria Kariakoo na Muhimbili kuanzia Mbezi, vivyo hivyo ifikirie uwezekano wa kuruhusu magari binafsi mengine zaidi kusafirisha wanafunzi kwa utaratibu utakaowekwa ili kupunguza usumbufu unaowapata hasa asubuhi na jioni.

Kwa hiyo jamii, serikali pamoja na wazazi hawana budi kuona namna bora ya kuwasaidia wanafunzi kipindi hiki ambacho shule zinaanza, lakini shida ya usafiri ikiwa haijatatuliwa kutokana na kuwapo kwa maradhi ya corona.

Ukosefu wa usafiri wa uhakika kwa wanafunzi umewakwamisha wengi kuwahi shuleni na pia umewachelewesha kuwahi vipindi vya asubuhi kutokana na kutopata usafiri kwa wakati.

Wapo wanafunzi wengine wa shule za watu binafsi wao changamoto hii inaweza ikawaepuka kwani wanausafiri wa mabasi ya shule ambayo huwawezesha kufika shule mapema ila kwa hawa wa shule za serikali usafiri kwao ni changamoto ambayo haijatatuliwa.

Ni wazi kuwa kuna baadhi ya shule zipo mbali na makazi kama wanaoishi Ubungo wanaosoma Kiluvya, licha ya kutumia usafiri wa mwendokasi hadi Mbezi kwa gharama ya Sh. 400, usafiri wa kuwafikisha Kibaha ni changamoto nyingine inayoweza kusababisha kushindwa kufika shuleni kwa wakati.

Wito wetu kwa serikali na wadau ni kuanza upya mchakato wa kuandaa magari maalumu kwa ajili ya kuwabeba wanafunzi ikiwamo hata kwa kutumia mabasi ya mwendokasi ambayo yanaweza kubeba wanafunzi wengi zaidi. Hili linaweza kufanikishwa baada ya kukamilika ujenzi wa barabara za mwendo kasi zinazounganisha sehemu mbalimbali za Dar es Salaam.

Kadhalika, utaratibu unaweza kufanywa katika miji na majiji mengine ili kufanikisha azma hiyo mikoani.


Kama ikizingatiwa mtazamo huu itasaidia wanafunzi kuwahi shuleni na kuepusha usumbufu wa usafiri na kusaidia kuboresha masomo yao.

Ni wakati pia wa kuandaa utaratibu wa kudumu wa kubeba wanafunzi kwani kwa miaka mingi ukosefu wa usafiri umewakwamisha wanafunzi wengi kusoma na hata kusababisha wafeli mitihani.

Hakishindikani kitu iwapo wadau wakiwamo wazazi, shule, serikali na taasisi nyingine zikiamua kutatua tatizo hilo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# *Unajua kupiga mswaki bila kusukutua, kinga ya meno?*

**MDOMO** unaelezwa na wataalamu wa afya, ni kiungo chenye mengi. Ila meno ndiyo yenye matatizo mengi, ambayo kuna wakati inasababisha watu kukosa raha na hata usingizi.

Mara nyingi dalili za kuumwa meno hujionyesha wazi na kwamba watu wengi hujijua kuwa tayari wana tatizo na huwa hawahitaji vipimo.

Dalili zake zinatajwa ni kuumwa meno wakati wa kula au muda wa baridi, joto, kutokwa na damu kwenye fizi, meno kuanza kulegea na kuachana na fizi, yote hayo yakionyesha kuwapo tatizo.

Pamoja na hilo, wataalamu wa afya ya kinywa wanasema meno ni muunganiko wa mfupa wa jino, fizi na mishipa, na kwamba kwenye kinywa cha binadamu kuna bakteria wanaoishi mdomoni wanaoitwa 'Normal Fraler'.

Kazi ya bakteria hao ni kutengeneza ute wenye acid unaolainisha chakula haraka mdomoni na pia wanasababisha ugonjwa unaoitwa 'gingivaites' unazifanya fizi kutoa damu pale mtu anapopiga mswaki.

Mtaalamu Dk. Festo Muhanga, anasema hali hiyo inapoachwa katika sura ya usugu, inaweza kusababisha ugonjwa unaoleta shida maradufu kwa mhusika.

Ni ugonjwa unaotajwa kwa jina 'machodifece' unaosababisha meno ama kuoza au kutoboka, kutokana na wadudu wanaoingia kwenye fizi kula damu.

Pia, wadudu hao wana kawaida kutumia vitu vyenye sukari kama pipi, chokoleti na juisi, zinazodaiwa kuchangia kuoza na kutoboka meno, baadhi ya watu wanang'oa meno yao, kutokana na maumivu yanayowakumba, pindi wanapoathiriwa.

Kuna ushauri kwamba, nyakati za usiku na wanapokula na kunywa, ni muhimu mtu akakasafisha kinywa na meno kwa kutumia mswaki, kwa ujumla walau mara mbili kwa siku.

Nikijikita kwenye ushauri unaotolewa na wataalamu hao, mara nyingi yote yanapokwama, mwisho wake ni kung'oa meno.

Pia, kuna mbinu mbadala kwamba mtu anapopiga mswaki hahitaji kusuuza mdomo kwa maji, kwa vile dawa inayobaki mdomoni inasaidia kuendelea kupambana na viini vinavyosababisha meno kuoza.

Hapa ndipo ninapotaka kujadili zaidi, kutokana na ukweli wengi wetu tunapopiga mswaki, huwa tunasuuza kwa maji na kisha na kutema, kumbe tunaondoa dawa inayosaidia kulinda meno yetu.

Msisitizo wataalam wa afya ya kinywa, wanasema mtu anaweza kupiga mswaki, akasuuza kwa mara ya kwanza na kutema, kisha akapiga tena mswaki akiwa na dawa na kuacha bila kusuuza.

Hivyo, ni wajibu wa kila anayelinda afya ya kinywa chake, angezingatia ushauri huo kwa ajili ya usalama wa meno yao kwa ujumla, kuepuka kung'oa, kinyume na dhana 'dawa ya jina ni kung'oa'.

Jambo la msingi, ni kwamba matatizo ya meno ni shida au magonjwa yanayohusiana na meno. Takriban matatizo yote ya meno, hutokea baada ya bakteria na wadudu wengine kuwepo mdomoni.

Kinachotakiwa kikuu ni kuzingatia maelekezo ya wataalamu waepuke maumivu makali kwenye meno, ambayo husababisha mtu kulazimika kwenda hospitali kung'oa.

Ni wazi kuna umuhimu mkubwa kila mtu akalinda afya ya kinywa chake, ili kusaidia kuepuka kuoza meno hata kusababisha yang'olewe, wabaki na mapengo au kuingia gharama nyingine na usumbufu wa meno bandia.

Ninasema hivyo, kwa sababu wapo baadhi ya watu ambao wamekumbana na tatizo la kuoza meno na kung'olewa na kubaki na mapengo, huku wenye uwezo kifedha wakiwekewa bandia.

Iwapo awali mtu alikuwa haumwi meno, lakini baadaye akakumbana na tatizo, ni vyema ajiulize ni kwanini na kisha majibu hayo yanamfanya achukue hatua zakufuata ushauri wa wataalam wa afya ya kinywa.

Mojawapo inajulikana, kupigwa mswaki mara mbili kwa kutwa, lakini kwa kutosuuza mdomo kwa maji, bali kutema dawa ya mswaki, dawa ikiachwa inaendelea kuua bakteria mdomoni.

HABARI KITAIFA

# UVCCM yamtetea Jecha kusaka urais CCM

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Vijana ya CCM (UVCCM), Kheri James, amesema kitendo cha kuchukua fomu za kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar, kwa waliokuwa watumishi ndani ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni haki yao kikatiba na hapaswi mtu kuwahukumu kwa chochote.

James, aliyasema hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uchaguzi mkuu mwezi Oktoba 2020, pamoja na uchukuaji fomu katika nafasi ya urais Zanzibar.

Alisema watu hawapaswi kutoa maneno ya kejeli pamoja na kuwashutumu wale ambao walikuwa watumishi wa serikali hiyo, ambao hivi sasa wameamua kuchukua fomu za kugombea urais wa Zanzibar.

Alisema kila mwananchi anayo haki kikatiba kugombea nafasi yoyote anayoona inafaa bila kuangalia kama alikuwa mtumishi wa umma au vinginevyo.

"Kumekuwapo na siasa za kuwakejeli, kuwashutumu watu waliochukua fomu za kugombea nafasi ya urais Zanzibar kwa sababu tu eti walikuwa watumishi wa serikali huko nyuma, hatutizami nyuma tunatizama haki ya kikatiba, na hakuna aliyevunja sheria mpaka sasa," alisema James.

Alisema katiba inamruhusu kila mtu kuchagua au kuchaguliwa na unyeti wa nafasi ya mtu aliyokuwa nayo katika utumishi wa umma haimnyimi haki ya kugombea hata kidogo.

"Tuwaache waliochukua fomu, wachukue kwani mchakato wa kuchukua fomu unajitegemea na ule wa kupembua majina ya wenye sifa unajitegemea hivi sasa ni mapema mno kuwashutumu watu, wapo waliokuwa viongozi wakuu ndani ya serikali na hivi sasa ni viongozi wakubwa katika vyama vya siasa nchini," alisema.

Mtumishi wa serikali wa zamani ambaye amekuwa akikosolewa sana na vyama vya siasa na makundi mengine ya jamii kwa kuchukua fomu za urais wa Zanzibar, ni Jecha Salim Jesha, ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC).

Jecha alifuta matokeo ya uchaguzi wa urais Zanzibar mwaka 2015 katika mazingira tata yaliyolalamikiwa na upinzani pamoja na baadhi ya waangalizi wa uchaguzi.

Wanaomkosoa Jecha wanatoa hoja kuwa hakupaswa kuchukua fomu kupitia chama chochote cha siasa, na kwamba kwa kupitia CCM, amedhihirisha kuwa alikuwa kada, hivyo hakutenda haki katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Aidha, akizungumza kuhusu wajumbe sita wa umoja huo Zanzibar, waliosimamishwa kupisha uchunguzi dhidi yao kutokana na kutuhumiwa kutoa na kupokea rushwa, alisema wamerudishwa katika nyadhifa zao baada ya kubainika kuwa wote hawana hatia.

Alisema kuwa uamuzi huo wa kuwasimamisha wajumbe hao, ulitokana na taarifa za kukamatwa kwao zilizotolewa na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA).




Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Annamringi Macha, akikabidhi baiskeli kwa watu wenye ulemavu katika Kata ya Bugarama na Bulyanhulu, kwa staili ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona kwa kutoshikana mikono, zilizotolewa na Mgodi wa Dhahabu wa Bulyanhulu, wilayani humo jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# MOI kuondoa uvimbe ubongo bila upasuaji

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), inatarajia kuanza kutoa huduma za uondoaji uvimbe kwenye ubongo bila kupasua fuvu.

Kuanza kwa huduma hiyo nchini, kutaifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache barani Afrika zinazotoa aina hiyo ya matibabu.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, alieleza mpango huo jana mbele ya Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, alipotembelea hospitali hiyo jana jijini Dar es Salaam na kuzungumza na wafanyakazi.

"Wiki chache kuanzia sasa tutaanza kutoa huduma ya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu la kichwa na kutaifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache barani Afrika zinazotoa huduma hii," alisema Dk. Boniface.

Alisema tayari serikali imeshanunua mitambo ya maabara ya upasuaji wa ubongo na kuisimika katika taasisi hiyo tayari kwa ajili ya kuanza kutoa huduma hizo za kibingwa.

"Uwepo wa maabara hii utatupa heshima kubwa kama nchi kwa sababu ni katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati hakuna maabara yenye vifaa vya kisasa kama hivi ambavyo serikali ya imenunua na kusimikwa hapa MOI, kwa hili tunamshukuru Rais John Magufuli," alisema Dk. Boniface.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano, MOI imeanzisha huduma nyingi za kibingwa na hivyo kumaliza rufani za kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi kwa matibabu.

"Tumeanzisha huduma nyingi za kibingwa kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali kwenye taasisi yetu, wiki iliyopita Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alizindua kituo cha kitaifa cha teleradiolojia hapa MOI," alisema Dk. Boniface.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Mollel, alisema serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya afya hususani kwenye huduma za kibingwa nchini.

Alisema kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali, taasisi ya MOI imeokoa zaidi ya Sh. bilioni 38.4 ambazo zingetumika kupeleka wagonjwa kufuata huduma za kibingwa nje ya nchi.

"Haya ni mafanikio makubwa ambayo lazima Watanzania wayafahamu kwamba serikali hii inawajali wananchi wake," alisema Dk. Mollel.

Kaimu Mkurugenzi wa Hospitali za Umma na Binafsi, Dk. Vivian Wonanji, alisema uwapo wa huduma za kibingwa nyingi nchini umechagizwa na mpango mkakati wa wizara wa mwaka 2017 ambao ulijikita katika kuboresha huduma za kibingwa ili kumaliza rufani za kupeleka wagonjwa nje ya nchi kwa matibabu.

# Lukuvi aagiza kuanzishwa daftari migogoro ya ardhi

**Na Mwandishi Wetu,** MANYARA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amezitaka ofisi za ardhi za mikoa zilizoanzishwa hivi karibuni, kuwa na daftari maalum lenye orodha ya migogoro ya ardhi, ili kurahisisha ufuatiliaji na utatuzi wa migogoro kwenye mikoa.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Ofisi ya Ardhi ya Mkoa mkoani Manyara jana, Lukuvi alisema kila ofisi ya ardhi ya mkoa inatakiwa kuwa na daftari zuri lenye orodha ya migogoro yote ya ardhi kwenye mkoa husika ikiwa ni mkakati wa kushughulikia migogoro ya ardhi nchini.

"Sasa hivi hatutegemei migogoro mipya maana migogoro tunayoshughulika nayo sasa ni ile ya miaka ya nyuma, hivyo muorodheshe migogoro yote iliyopo wilayani na kuanza kuishughulikia," aliagiza.

Waziri Lukuvi alishangazwa na ofisi za ardhi katika halmashauri za wilaya nchini kushindwa kutatua migogoro ya mipaka baina ya wilaya na wilaya wakati halmashauri hizo zina wataalamu wa sekta ya ardhi wanaoweza kuitafsiri GN.

Katika hatua nyingine, Lukuvi ameagiza kufanyika ukaguzi wa mashamba makubwa yaliyomilikishwa kwa wawekezaji mkoani Manyara, ili kubaini mashamba yasiyoendelezwa.

Alitoa agizo hilo baada ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, kueleza kuwa mkoa huo una mashamba makubwa yasiyoendelezwa kwa muda mrefu wakati uhitaji wa mashamba kwa wananchi wa mkoa huo ni mkubwa kutokana na ongezeko la idadi ya watu.

"Hatujatoa ardhi kwa ajili ya kuweka akiba, kazi ya ukaguzi wa mashamba ni ya kwenu, hivyo myaangalie kama yameendelezwa, yana faida gani na yanalipa kodi?" Lukuvi aliagiza.

Mnyeti aliwapongeza watumishi wa sekta ya ardhi katika mkoa wake kwa kufanya kazi kwa utii na nidhamu, tofauti na ilivyokuwa huko nyuma kwa watumishi wa sekta hiyo.

Mnyeti aliongeza kuwa Mkoa wa Manyara umekuwa na tatizo la wananchi kuvamia maeneo ya umma kutokana na kukosekana hati miliki za maeneo hayo na hivyo kutoa mwanya maeneo hayo kuvamiwa.

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mary Makondo, alisema wizara yake imefanikiwa katika suala la usimamizi rasilimali ya ardhi, huku lengo likiwa kutaka kupima kila kipande cha ardhi na kuwamilikisha wananchi.

# Majaliwa aahidi utatuzi wa changamoto bila ubaguzi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali itaendelea kushughulikia changamoto mbalimbali zinazowakabili Watanzania wote zikiwamo za afya, maji, miundombinu na elimu bila ya kujali itikadi zao.

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana alipozungumza na wananchi baada ya kutembelea zahanati ya kijiji cha Nandagala akiwa katika ziara ya kikazi Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, ambapo amewataka wananchi washikamane na serikali katika kuboresha maendeleo yao.

"Suala la maendeleo halina chama, maendeleo yaliyoletwa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ni kwa ajili ya wananchi wote, hivyo watu wote tunatakiwa tushikamane kwa pamoja kumshukuru na kumuunga mkono Rais Dk. John Magufuli kwani shule, hospitali anazojenga zinatumika na watu wote."

Amesema wananchi wanatakiwa watambue jitihada kubwa zinazofanywa na Rais Dk. Magufuli katika kuboresha huduma za afya. "Leo nimeshuhudia wagonjwa wakiwa wamelazwa katika zahanati yetu ya Nandagala. Haya ni mafanikio makubwa awali hatukuwa na zahanati hapa."

Alisema awali kijiji hicho hakikuwa na zahanati na wakazi wake waliuguzwa majumbani kwa kushindwa kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya, ujenzi wa zahanati hiyo umekuwa mkombozi mkubwa hususani kwa wajawazito kwani huduma zote zikiwamo za mama na mtoto zinatolewa hapo.

Vilele, alitembelea kijiji cha Luchelegwa na amekabidhi gari la kubebea wagonjwa katika Kituo cha Afya cha kata ya Luchelegwa. Gari hilo limetolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ufadhili wa Global Fund.

Aliwaagiza viongozi wa vijiji vyote ambavyo havina zahanati viongozi wake waanzishe miradi ya ujenzi wa zahanati na watakapokamilisha ujenzi wa maboma serikali itawapelekea vifaa vya viwandani yakiwamo mabati na misumari.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Luchelegwa, Dk. Codratus Mutabihirwa, aliishukuru serikali kwa kuwapa gari la kubebea wagonjwa kwani awali walikuwa wanapata tabu pale wanapokuwa na mgonjwa anayetakiwa kuhamishiwa hospitali ya wilaya.

Alisema gari hilo litatumika kwa matumizi yaliyokusudiwa na kwamba watalitunza ikiwa ni pamoja na kuhakikisha linakuwa na mafuta wakati wote.

Nao baadhi ya wananchi wa kijiji cha Luchelegwa waliishukuru serikali kwa kuwapatia gari la kubebea wagonjwa kwa sababu walikuwa wanapata tabu sana hususani kwa wajawazito ambao walikuwa wakihamishiwa hospitali ya wilaya kwani walikuwa wanatumia pikipiki.

Sauda Kaisi, aliushukuru serikali kwa kuwapelekea gari hilo kwa kuwa Kituo cha Afya cha Luchelegwa hakikuwa na gari la kubebea wagonjwa jambo ambalo lilisababisha baadhi ya ndugu zao kupoteza maisha kwa kushindwa kupata huduma kwa wakati.

Joyce Chimela alimshukuru Rais Magufuli kwa uboreshaji wa huduma mbalimbali kwenye wilaya yao kikiwamo Kituo chao cha Afya cha Luchelegwa ambacho kimepewa gari la kubebea wagonjwa litakalowafikisha kwa wakati hospitali ya wilaya.



Waziri wa Afya, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (katikati), akipata maelezo ya ujenzi wa jengo la kituo cha tiba cha waathirika wa dawa za kulevya katika Hospitali ya Mkoa wa Tanga Bombo jana, wakati wa uzinduzi wa huduma za methadone katika Siku ya Maadhimisho ya Kupinga Matumizi ya Dawa za Kulevya. **ICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# 'Mfumo dume chanzo wajane kunyanyaswa'

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

KAIMU Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, amesema malalamiko mengi yanayowakuta wajane nchini hutokana na mfumo dume ulipo katika baadhi ya jamii unaosababisha wengi wao kukosa haki za kumiliki mali pindi wenza wao wanapofariki dunia.

Clemence Mkusa aliyasema haya jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu Siku ya Wajane, akiitaka jamii kuachana na vitendo vya kunyanyasa wajane na wanawake kwa ujumla.

Alisema mfumo dume uliopo katika baadhi ya jamii nchini umekuwa tatizo kubwa kwa kundi hilo kwa kuwa haki za wanawake zimekuwa zikiminywa, ikiwa ni pamoja na kudhulumiwa mali walizozitafuta na waume zao na kusababisha familia kuishi maisha duni.

Alisema wajane hunyanyaswa kwa kiasi kikubwa na wengine huachwa wakiwa na watoto ambao hukosa haki ya elimu, kunyang'anywa mashamba, nyumba na mali zingine.

Aliitaka jamii kuisaidia serikali kuwaibua kinamama wajane walionyang'anywa mali na kunyanyaswa katika maeneo ya pembezoni, ili wapate msaada wa kisheria.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Mji wa Kahama, Robert Kwela, alisema wajane wanakumbana na mtatizo mengi kimaisha ikiwa ni pamoja na ya kisheria na upatikanaji wa fursa za kiuchumi katika maeneo waliko.

Alisema kuwa kutopatikana kwa fursa nyingi za kiuchumi, kumesababisha wajane wengi kutojishughulisha na shughuli za kimaendeleo, hivyo wenzi wao wanapofarikia dunia, hupata tabu ya kimaisha kutokana na kutokuwa na mradi wowote.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alisema kwa sasa serikali iko macho katika kuhakikisha wanawake, hususan wajane, hawanyanyaswi.

"Wanaume wengi wanamiliki mali bila ya kuwashirikisha wenza wao, hali ambayo pindi wanapofariki dunia, mali hupotea kwa urahisi mikononi mwa watu wasiokuwa ndugu wa marehemu," alisema.

# Wafanyakazi Regency wamkumbuka Dk. Kanabar

**Na Joseph Mwendapole**

WAFANYAKAZI wa Hospitali ya Regency wamemkumbuka mwanzilishi wa hospitali hiyo, Dk. Rajni Kanabar kwa kuahidi kuendeleza mambo mema aliyoyafanya hasa kusaidia watu wakati leo akitimiza mwaka mmoja tangu afariki dunia.

Dk. Kanabar ambaye ni mwanzilishi na Mwenyekiti wa hospitali hiyo alifariki Juni 25, mwaka jana.

Akizungumza hospitalini hapo jana, mtaalamu wa magonjwa ya figo, sukari na shikizo la damu, Dk. Emmanuel Maganga, alisema hatamsahau Dk. Kanabar kwa namna alivyogusa maisha yake.

Alisema kutokana na ucheshi na upole wake alizoea kumuita babu kwa sababu aliwalea kama wajukuu zake kwa kuwaelekeza kwa upole hata anapokosea.

Dk. Maganga alisema Dk. Kanabar alimsaidia kwenda nje ya nchi kusomea shahada mbili na aliporejea aliendelea kufanyakazi Hospitali ya Regency na kumpa nafasi mbalimbali hospitalini hapo.

"Alihimiza sana upendo na hata ukiwa na mambo binafsi ya kufamilia alisikiliza na kutatua hapohapo, ni viongozi wachache ambao unaweza kumsubiri getini ukamweleza shida yako na akaitatua hapo hapo babu aliweza hilo," alisema Dk. Maganga.

Muuguzi Mkunga hospitalini hapo, Judith Mahandela, alisema wanamkumbuka Dk. Kanabar alivyoishi nao bila ubaguzi wala upendeleo na alivyojali maslahi ya wafanyakazi wake.

Alisema kupitia Dk. Kanabar mradi aliousimamia wa Heart Babies, watoto wengi Watanzania wenye matatizo mbalimbali ya moyo walipata nafasi ya kwenda kutibiwa bure nchini India na kurejea wakiwa na tabasamu.

# Wananchi waanzisha shule kukabili msongamano

**Na Sara Magesa,** GEITA

WANANCHI wa Kijiji cha Nyarututu, Kata ya Bwanga wilayani Chato, wamelazimika kuanzisha shule sitiri ili kupunguza msongamano wa wanafunzi katika shule mama ya Nyarututu.

Shule ya Msingi Nyarututu yenye wanafunzi 6,500 ina madarasa 11 na kusababisha wanafunzi zaidi ya 500 kutumia chumba kimoja cha darasa.

Wazazi wa kijiji hicho wakipokea msaada wa vifaa vya ujenzi vilivyotolewa na wakala wa misitu nchini kupitia Shamba la Misitu Biharamulo, walisema uamuzi huo ni kuwasaidia wanafunzi wao.

HABARI KITAIFA

# Miradi mikubwa yahamasisha w'biashara kulipa kodi kwa wakati

**Na Gwamaka Alipipi**

WAFANYABIASHARA Mkoa wa Tanga wamesema hawaoni shida ya kulipa kodi kwa wakati baada ya kuona utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo inayofanywa katika uongozi wa Rais John Magufuli kupitia kodi zao.

Waliyasema hayo wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi, inayofanywa na maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutoka Makao Makuu wakishirikiana na maofisa wenzao kutoka mkoa huo.

Maofisa hao waliwatembelea wafanyabiashara kwenye maduka yao yaliyopo barabara za namba jijini Tanga, kwa lengo la kuwaelimisha na kuwakumbusha kulipa kodi kwa wakati.

Maofisa hao pia walisikiliza kero zinazowakabili wafanyabiashara hao na kusikiliza maoni yao kama mpango wa kutengeneza mazingira rafiki kati yao na TRA.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Thabiti Salimu, kutoka eneo la barabara za namba, alisema litakuwa jambo la ajabu kwa mfanyabiashara kukwepa kulipakodi katika utawala wa sasa hususan katika kipindi hiki ambacho miradi mingi ikitekelezwa kupitia makusanyo ya kodi.

"Rais Magufuli anatumia kodi zetu vizuri, tunaona utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo, hivyo lazima tuendelee kulipa kodi la sivyo kazi ya utekelezaji wa miradi hii itakwama," alisema Salimu.

Salimu alipongeza mpango ulioanzishwa na mamlaka hiyo wa kuwatembelea wafanyabiashara na kuwasikiliza, akisema ni mpango mzuri ambao unapaswa uendelee kutokana na umuhimu wake kwa ustawi wa mlipakodi.

Mfanyabiashara mwingine, Dina Mbenu, ambaye anauza vipuri vya pikipiki, alisema ikiwa wafanyabiashara watakwepa kulipa kodi watasababisha madhara ya kiuchumi na kuathiri jitihada za Rais za kuboresha miundombinu ikiwamo barabara.

Alisema hatua ya maofisa wa TRA kuwatembelea kwenye maduka yao kwa lengo la kuwahamasisha kulipa kodi na kusikiliza kero na maoni yao, inawasaidia kutopoteza muda kwenye ofisi za TRA wakisubiri kuhudumiwa.

Naye Ofisa Msimamizi Mkuu wa Kodi, Julius Mjenga, alisema mchakato wa kuwatembelea wafanyabiashara ni endelevu na kabla ya kufanyika Tanga, zoezi hilo limeshafanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Morogoro.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kutoa elimu ya kodi, kuwakumbusha wafanyabiashara kulipa kodi kwa wakati, kusikiliza maoni yao pamoja na changamoto kwa ajili ya kuzitatua.

Meneja wa TRA Mkoa wa Tanga, Specioza Owure, aliwaomba wafanyabiashara kuunga mkono zoezi linalofanywa na maofisa wa TRA la utoaji elimu ya kodi, kusikiliza maoni na changamoto zao kwa kuwa zoezi hilo linalenga kuboresha huduma kwa mlipakodi.

Alisema: "Niwaombe wafanyabiashara wote mkiwaona maofisa wanatembelea, msifunge maduka, wapokeeni na kuwapa ushirikiano kwa kuwa wanalenga kuwaelimisha na kuondoa changamoto mbalimbali zinazowakabili kwenye biashara zenu ambazo kwa pamoja tunaweza kuzitafutia ufumbuzi."



Ofisa Programu Idara ya Habari ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Monica John, akizungumza na waandishi wa habari kwenye warsha kuhusu bajeti yenye mlengo wa kijinsia, iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mazao ya mikunde ya Dola mil. 70 yauzwa nje wakati wa corona

**Na Beatrice Philemon**

KUTOFUNGIA watu ndani wakati wa ugonjwa wa virusi vya corona nchini kumesaidia Tanzania kuuza mazao ya jamii ya mikunde yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 70 katika nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu, India, Uganda na Kenya kuanzia Januari hadi Mei mwaka huu.

Hayo yalisemwa jana na Mshauri wa Sera na Mipango, Mtandao wa Mazao ya Jamii ya Mikunde (TPN), Junior Ndesanjo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu sekta ya mazao ya jamii ya kunde Tanzania na matokeo ya ugonjwa wa COVID-19 wakati raia wa nchi nyingi duniani walipoamriwa kujifungia ndani.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kutoweka 'lockdown' hapa nchini na kuruhusu tufanye biashara kwa sababu wafanyabiashara wengi Tanzania wamefanikiwa kuuza kunde, choroko, mbaazi, maharage na dengu nchini India na mashariki ya mbali na kuinua kwa kiasi kikubwa sekta yetu ya mazao ya jamii ya mikunde," alisema.

Alisema kutokana watu kujifungia ndani katika nchi mbalimbali duniani zikiwamo India, Kenya, Canada na zingine, Tanzania ilitumia nafasi hiyo kuuza mazao yake.

Pia wameishukuru Bandari ya Dar es Salaam kwa kuwapa ushirikiano mzuri wakati wa kusafirisha mazao yao, na kuwa sasa hivi masoko mengi ya mazao ya jamii ya mikunde yameongezeka na yanazidi kuongezeka.

"Tunategemea masoko kuongezeka hadi asilimia 48 mwaka huu kutoka asilimia 20 kwa sababu uzalishaji wa mazao haya India siyo mkubwa mwaka huu kutokana na kizuizi," alisema.

Alisema kutokuwapo kizuizi kumesaidia Tanzania kuwa na masoko makubwa katika nchi za mashariki ya kati.

## Tuzo za waandishi SADC kufanyika Agosti

**Na Magdalena Haule, UDOM**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, amesema kuwa tuzo kwa waandishi bora wa habari za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) zitafanyika Agosti mwaka huu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, alisema tuzo hizo zitahusisha magazeti, redio na runinga.

Alisema tuzo hizo zitafanyika Msumbiji na kujumuisha wanahabari mbalimbali kutoka nchi wanachama.

"Ratiba ya kazi za kamati ya kutafuta washindi wa tuzo za habari inawapa siku mbili kupata washindi katika maeneo manne ambayo ni picha, redio, televisheni na magazeti," alifafanua Mwakyembe.

Aliongeza: "Tanzania katika nafasi yake ya uwenyekiti wa SADC ilikuwa imejipanga kuandaa mkutano huu uliokuwa ufanyike Dar es Salaam, lakini kwa bahati mbaya kutokana na ugonjwa wa corona, ipo tayari kuongoza kikao hiki ili kuhakikisha washindi wa habari wa SADC wanapatikana."

Katika hatua nyingine, waziri aliwapongeza waandishi wa habari kwa kutekeleza kikamilifu jukumu lao la kusambaza taarifa sahihi na za ukweli kwa umma kuhusu mwenendo wa corona.

"Kazi ya kuelimisha umma kipindi cha janga la corona imekuwa nzuri sana inayohitaji kuthaminiwa na kwa wanachama wa SADC," alisema Waziri Mwakyembe.

## DC ataka vifaa vya hospitali Mkuranga

**Na Julieth Mkireri, MKURANGA**

MKUU wa Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, Filberto Sanga, amemwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Mshamu Munde, kuhakikisha uwapo wa vifaa mbalimbali katika hospitali ya wilaya hiyo vikiwamo kompyuta ambavyo vitachochea kwenye utoaji huduma bora.

Sanga alitoa rai hiyo wakati akizungumza na madaktari, wauguzi sambamba na baadhi ya wananchi kwenye hafla ya kukabidhi kompyuta tano na printa kwenye Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga zilizotolewa na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega.

Alimpongeza Naibu ambaye ni mbunge anayemaliza muda wake katika Jimbo la Mkuranga, kwa kusaidia kwa vifaa hivyo ambavyo vitarahisisha utendaji kwa wahudumu wa afya wa hospitali hiyo.

Sanga pia aliwataka wananchi vijiji vyote vya wilaya hiyo kuendelee kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya katika kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa corona.

Munde alimtaka Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Stephen Mwandambo, kuhakikisha utamaduni wa zamani wagonjwa kusubiri muda mrefu kupokea taarifa kwa waganga unaondoka kufuatia upatikanaji wa kompyuta hizo.

# NEMC kutafiti ongezeko kina cha maji cha Ziwa Victoria

**Na Mwandishi Wetu, BUKOBA**

MWENYEKITI wa Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Prof. Esnat Chaggu, ameiagiza Menejimenti ya Baraza hilo kufanya utafiti ili kubaini sababu zinazochangia kuongezeka kwa kina cha maji katika Ziwa Victoria, na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kukabiliana na kuepuka athari za mafuriko.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye ziara ya wajumbe wa bodi hiyo na Menejimenti ya Baraza kujionea athari za kuongezeka kwa kina cha maji katika Ziwa Victoria na kusababisha mafuriko katika baadhi ya maeneo na kuharibu miundombinu, Prof. Chaggu alisema NEMC ipo kwenye nafasi nzuri ya kufanya utafiti na kuja na mapendekezo ya kukabiliana na mafuriko.

"Taarifa za utafiti uliofanyika muhimu zitafutwe na yachukuliwe mapendekezo ambayo yatatuwezesha kupata mwelekeo wa namna ya kukabiliana na hali iliyotokea na kufanya utekelezaji," alisema Prof. Chaggu.

Aliongeza kuwa ushirikiano zaidi unahitajika katika kufanikisha utafiti utakaotoa sababu za kuongezeka kwa kina cha maji katika Ziwa Victoria, hivyo kuna kila sababu ya kufanya hivyo sasa.

"Ziwa hili limeingia katika nchi za Kenya na Uganda, hivyo ni muhimu mamlaka zetu zikashirikiana na mamlaka za nchi hizo jirani ili tuwe na nguvu ya pamoja kunusuru hali iliyojitokeza isilete athari zaidi miaka ijayo," alisema Prof. Chaggu.

Alisema faida zitokanazo na Ziwa Victoria ni kubwa katika nchi zote zinazozungukwa na ziwa hilo na hivyo kuna kila sababu za kuunganisha nguvu katika kulilinda kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadaye.

"Mabadiliko ya tabia nchi, kujaa kwa tope ndani ya ziwa kutokana na shughuli za binadamu katika maeneo ya vyanzo vya maji kunaweza kuwa ni sababu, hivyo tafiti ni muhimu nalo likaangaliwa," alisema.

Aidha, Prof. Chaggu aliyetoa wito kwa wawekezaji na wananchi wanaoishi karibu na ziwa kabla ya kufanya mradi wowote wa kimaendeleo ikiwamo kujenga makazi, ni vizuri wakapata mwongozo wa kufanya tathmini ya athari kwa mazingira (EIA) kabla ili kuepuka hasara endapo tatizo litatokea katika eneo husika.

Diwani wa Kata ya Miembeni Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, Richard Mwemezi, alisema hali ya kujaa kwa kina cha ziwa hakijawahi kutoka na athari zilizojitokeza ni kubwa na kusababisha wananchi kuhama makazi yao.

"Tunaomba serikali itutengenezee miundombinu ya barabara ili tuweze kuendelea na shughuli za kutuingizia kipato kwenye soko kubwa la samaki lilipo katika eneo hili ambalo limeingiliwa na maji na kufanya biashara kusimama," amesema Mwemezi.

# Waathirika wa ukatili wa kijinsia waishangaa jamii

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

WAATHIRIKA wa matukio ya udhalilishaji Wilaya ya Mkoani Pemba, wamesema wanaishangaa jamii kuwatenga, kuwagomea na kuwanyooshea vidole wanapozisimamia kesi za udhalilishaji baada ya kukataa suluhu.

Walisema jamii imekuwa ikiwawekea vikao vyenye lengo la kusimamisha kesi hizo hasa ambazo watendaji ni watu maarufu kama masheikh, walimu wa madrasa, kwamba zisifikishwe Polisi na zifanyiwe suluhu katika ngazi ya jamii.

Wakizungumza kwenye kikao maalum cha kujengewa uwezo wa kutoa ushahidi mahakamani na hatua za kupita baada ya kutokea tukio hilo, kilichoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) ofisi ya Pemba, walisema kikwazo kikubwa ni jamii.

Walisema, kwa mfano unapoiripoti kesi ya udhalilishaji kituo cha Polisi hufuatwa na familia na hata jamii kwa makundi, kuwa kesi hiyo isifikishwe polisi kwani hilo ni bahati mbaya.

Mmoja kati ya wazazi hao ambao mwanawe wa miaka 14 alibakwa kutoka shehia ya Kangani, alisema alifuatwa kuwa kesi hiyo aachane nayo na atapewa kiasi cha fedha atakacho.

Alisema, baada ya kuonekana kuwa na msimamo, alitumwa sheikh ili azungumze na mumewe aachane na kesi hiyo, kwani lililojitokeza ni bahati mbaya.

"Nilishangaa jamii yote ilinizunguka kwamba nilichokifanya cha kumpeleka kijana aliyenibaka mwanangu polisi, sio uungwana, bora ningekubali kuchukua fedha ili mambo yaishe," alisema.

Naye mzazi kutoka Shehia ya Ng'ombeni ambaye mwanawe alibakwa miaka tisa iliyopita, alisema amesuswa na jirani zake na jamii kwa ujumla, kwa sababu ya msimamo wake.

"Mwanangu alibakwa tokea yuko darasa la nne na sasa yuko darasa la kumi 11, lakini nikifuatwa nakataa kufanya suluhu, na washatumwa watu wenye hadhi tofauti, lakini sijakubali," alieleza.

Mwanamke aliyetaka kubakwa na rafiki wa mumewe majira ya saa 7:15 usiku eneo la Kangani, alisema kwanza sheha alitaka kuongoza kikao cha suluhu kwa madai kuwa kesi hiyo ikifikishwa Polisi anaweza kusababisha mfarakano.

Mratibu wa TAMWA ofisi ya Pemba, Fat-hiya Mussa Said, aliwataka wahanga hao kuwa na msimamo wa dhati, wakijua kuwa kufanya hivyo ni kutetea haki za watoto wao.

Alisema kama jamii inawapenda watuhumiwa wa makoasa ya udhalilishaji, ni vyema wakawapa elimu ya kuacha matendo hayo na sio kusubiri baada ya tukio ndio wakawabeba.

Alieleza kama mwalimu wa madrassa, sheikh, mwalimu wa shule, kiongozi mkuu kwenye taasisi yoyote anaogopa kuvunjiwa heshima, kwanza aanze yeye kuwaheshimu watoto wa wenzake.

"Haiwezekani hata kidogo kuwa mtu ameshabaka au kulawiti na kisha aonewe huruma na kwamba akipelekwa Polisi atavunjiwa haki zake, bali aanze yeye kuchunga haki za wengine," alieleza.



Mkurugenzi wa kampuni ya nguzo za umeme ya Qwihaya General Enterprises, Leonard Mahenda, akitoa taarifa ya kiwanda hicho, kwa Waziri wa Uwekezaji, Angella Kairuki (kushoto), alipotembelea kiwanda hicho mjini Mafinga, mkoani Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Mil. 780/- kuwainua kinamama, wajane

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

HALMASHAURI ya mji wa Kahama, imetenga na kutoa kiasi cha shilingi milioni 780.6 kwa vikundi vya kinamama wakiwamo wajane kwa kipindi cha miaka minne kwa ajili ya kuwainua kiuchumi na kuondokana kuwa tegemezi kwenye familia zao.

Abrahamani Nuru, Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri hiyo, aliyabainisha hayo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wajane nchini, na kuhudhuriwa na Mkuu wa Wilaya Anamringi Macha, Dawati la jinsia, mashirika yasiyo ya kiserikali ya Huheso Foundation na TEDEPHA.

Alisema mwaka wa fedha 2016/17 halmashauri ilitenga kiasi cha shilingi milioni 97.6 na kutoa mkopo huo kwa vikundi 58 vya kinamama, huku kipaumbele wakipewa wajane na fedha hizo zinatokana na kwamba mapato ya ndani ya halmashauri.

Pia Nuru alisema mwaka 2017/18 halmashauri ilitenga kiasi cha shilingi milioni 102.5 na kutoa mikopo isiyokuwa na riba kwa vikundi vya kinamama 34 katika kata 20 zinazounda halmashauri hiyo.

Aidha, alisema mwaka 2018/19, halmashauri ilitenga na kutoa kiasi cha shilingi milioni 342.5 na kutoa mkopo huo kwa vikundi vya kinamama na wajane 104, huku mwaka 2019/20 ikitenga kiasi cha shilingi milioni 238 kwa vikundi 76.

Alisema mwaka 2019/20 walipokea mashauri ya kunyanyaswa wanawake na watoto wadogo 1,622, wajane wakiwa 604, huku watoto chini ya miaka 18 wakiwa 158.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Clemensi Mkusa, alisema malalamiko mengi ya wajane yapo kwenye migogoro ya ardhi wakati anapofiwa na mwenza wake, kwamba na wengi wanaonyanyasika hawatambui wapi wanapata haki zao.

DC Macha alisema kitendo cha familia kutoandika wosia kwa mrithi wake anapofariki dunia ndio sababu ya wajane kudhulumiwa mali na watoto kuhangaika mitaani.

Hata hivyo, alisema kuwa, hatasita kuwachukulia hatua za kisheria wale wote watakaohusika kuingilia na kudhulumu mali za wajane.

# ama

ALHAMISI JUNI 25, 2020

AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

**Mambo ya ndani yanayomhusu mdudu mbu, hatari zake zilivyo**



Ukurasa 13

Kauli za mashuhuda walioondolewa mawe tumboni bila kufanya upasuaji



Ukurasa 14

**Uvamizi kuni za kupikia msituni unavyoitafuna Hifadhi ya Jozani**

AFYA

# Timiza Malengo 2020; kampeni inayonuia kuvusha vijana kiafya

**Na Mwandishi Wetu**

HADI sasa inajulikana vijana nchini ni wahitaji wa msukumo na usimamizi kutoka kwa jamii, wazazi na serikali waweze kusoma na kujifunza stadi za maisha kufikia malengo na ndoto zao katika utu uzima.

Ndio hatua inayoibua Shirika la Vijana (TAYOA) kuelekea kampeni ya Timiza Malengo 2020, mtazamo wa vijana wasiachwe bila jamii kuwasimamia kwa karibu wasipotoke, kwani jirani walipo kuna adha za ulevi, uvutaji bangi na ngono zisizo salama.

Katika hilo, TAYOA imeanzisha programu zinazolenga kuwawavuta vijana kwenye msitari wenye manufaa kwao na jamii zinazowazunguka, familia na taifa, hata wakafikia ndoto njema za kuijiriwa, kujiajiri na kuwaajiri wengine.

Wiki iliyopita, asasi hiyo kwa ufadhili wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Mpango wa Taifa wa Kupambana na Ukimwi (NACP), kupitia mradi unaoitwa Global Fund, zikifanya mdahalo unaopitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama), kukiwepo orodha ya wadau wengime wengi.

Hapo walishirikishwa zaidi ya wanavyuo weasiopungua 680, kutoka taasisi 32 za elimu ya juu nchini, maudhui yakizama katika kutimiza ndoto, huku wakijihami na maambukizi ya virusi vya Ukimwi.





Mjadala wa njia ya mtandao ukiendelea kuhusu vijana na hatima yao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

**MKURUGENZI TAYOA**

Mkurugenzi wa Tayoa, Peter Masika, anasema kufanikishwa mdahalo huo ni ushahidi wa kutosha kwamba kwamba Tehama inaweza kutimika kuleta mabadiliko, kwani kilichofanyika kwa wana vyuoni wa mikoa tofauti kimeonyesha mfano.

Anasema, TAYOA inaendesha kampeni hiyo kuhamasisha vijana na wanafunzi, wanaopaswa kuwa na malengo wanayotatekeleza, ikiwamo tabia ya vijana kuwa na tabia ya kujitafutia maarifa na stadi mbalimbali.

Mkurugenzi huyo anasema, asasi hiyo imejiwekea utaratibu wa kuendesha midahalo kama hiyo kila mwezi, inayowajenga vijana kiafya na kuwa wajasiriamali watakaotengeneza ajira mpya na kodi za kiatifa, inayoipa maendeleo endelevu.

**TUME UKIMWI**

Jeremiah Mushi, kutoka Tume ya Ukimwi anawataka vijana kuwa makini dhidi ya maambukizi virusi vya Ukimwi (VVU), akirejea takwimu zilizopo, kila dakika moja inayopita ina Watanzania wanne wanaombukizwa; kwa siku wako 200; kila mwezi watu 6,000; na mwaka wastani watu 72,000.

Kwa mujibu wa Mushi, hadi sasa kuna Watanzania milioni 1.7 waliothibitika kuambukizwa na asilimia 95 kati yao wanatumia dawa za kufubaza virusi. Eda Charles, wa Tume ya Ukimwi, anasema kuna wasichana wengi wanaoangukia ujauzito na hata washindwa kutimiza ndoto zao, kutokana na mazingira magumu ya masomo kama vile kutembea umbali mrefu.

Anasema, watu wenye nia mbaya huwalaghai kimasomo na wanaangukia katika mimba na kuambukizwa VVU, jambo linalowasukuma wao wadhibiti Ukimwi kuingilia kati kwa kuwaamsha wasichana wajitambue.

Anasema mbali na hayo, wamekuwa wakiwapa elimu ya ujasiriamali waweze kujitegemea, kwani waliona kwamba utegemezi unaweza kuwa chanzo cha manyanyaso kwa wasichana na kuwakatisha ndoto zao.

Kwa mujibu wa Eda, nia imejikita katika kuwawekea mazingira mazuri na utulivu shuleni, wasikutane na vishawishi vya wanaume wanaotumia changamoto kuwa fursa za kuwalaghai.

**MRATIBU UMATI**

Mratibu wa Chama Cha Uzazi na Malezi Bora Tanzania (UMATI), Fredy Turuka, anasema utata uliopo, vijana wanaogopa mimba, lakini wanadharau kuvaa kinga za usalama katika tendo la kujamiiana.

"Wakati wanapofanya mapenzi wanazingatia sana kutopata mimba, kuliko Ukimwi. Wamekuwa wakisema hawasikii ladha ya tendo," anaeleza na kutaja kuwa mzizi wa hatari uliojificha.

Turuka anaikumbusha jamii, wajibu wa kuwalinda vijana kufikia ndoto zao za kimaendeleo na wanawajibika kujihami kwa ngono salama na wakati unaokubalika.

"Vidonge vya kuzuia mimba kama vinaweza kutumika tu katika hali ya dharura, lakini si kila mara, kwa sababu lile tukio siyo la dharura na limepangwa, basi wahusika wajikinge na mimba zisizotarajiwa kwa kutumia njia salama badala ya vidonge," anafafanua.

Turuka anaikumbusha jamii iwekeze zaidi kwenye afya ya vijana, ili wanapomaliza masomo yao waweze kuwa na manufaa kwa jamii na taifa lao, badala ya kuwa mzigo kama ambavyo uzoefu uliopo unaonyesha.

Anasema serikali imewekeza fedha nyingi kwenye miundombinu ya elimu kama majengo, walimu, maabara kulipa mishahara, hivyo haipaswi kusahau uwekezaji kwenye afya ya vijana wanaotumia miundombinu hiyo, ili mtazamo wa jumla ubebe manufaa ya sasa na baadaye.

Ofisa huyo mtaalamu wa UMATI, anahitimisha kwa msisitizo:"Hawa(vijana) ni wenzetu kwenye maendeleo. Kama tutaangalia sana miundombinu na tukawasahau, tutakuwa tumefanya makosa makubwa sana, kwa sababu kijana anaweza kumaliza shule akawa ameathirika au ametumia dawa za kulevya asiwe na manufaa tena."

AFYA

MTAALAMU WA MBU:

# Mambo ya ndani yanayomhusu mdudu huyo, hatari zake zilivyo



Alphonce Assenga, Ofisa Utafiti katika Taasisi ya Afya Ifakara.



Mbu aenezaye maradhi ya dengue.



Huyu ndiye mbu aenezaye malaria. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

**Na Beatrice Philemon**

DUNIANI kuna zaidi ya aina 3500 za mbu, japo takribani kuna aina 100 za wasambazaji magonjwa kwa binadamu, Nipashe inaainishiwa kupitia faragha maalum na mtaalamu wa afya ya binadamu nchini.

Alphonce Assenga, Ofisa Utafiti katika Taasisi ya Afya Ifakara (IHI), anaendelea kuwa mbu hao ni hatari sana kwa afya ya mwanadamu na viumbe vingine, wakitishia maisha yao na ndio maana kuna hatua nyingi za kibinadamu kumuangamizi kiumbe huyo.

Katika ufafanuzi wake, anasema mbu wanapatikana zaidi katika maeneo ya kitropiki na yale yanayofanana nayo (sub-tropical), ambako hali ya hewa na mazingira yanawavutia kuishi.

Mtafiti mtaalamu huyo, anasema mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea kushuhudiwa yana mchango katika mbu wanaoshamiri, hali inayopanua wigo wa maeneo yao kuishi, ambayo katika upande wa pili wa shilingi, ni mzigo na janga kwa mwanadamu.

**MBU ANAUMAJE?**

Mtaalamu Assenga anajibu hoja hiyo, kwa kuambatanisha na ufafanuzi wa umuhimu kutambua si mbu wote wanaowauma binadamu, kwani kuna wengine wanawauma wanyama.

Pia, anasema mbu anamuuma binadamu au mnyama, ingawa dhamira yao si kama iliyoko katika tafakari ya wanadamu, kwani wao huuma kwa nia ya kupatia damu anayotumia kutaga na kukuza mayai yake.

> **“ Mbu aenezae malaria anaelezwa mazalia yake, ni pamoja na madimbwi mbalimbali ya maji kama yaliyoko kwenye maoteo ya mpunga yatokanayo na mafuriko, maji yaliyochepuka miferejini, kando ya mito na**

Assenga anataja lingine, kwamba katika kundi hilo la mbu wanaouma binadamu, sehemu kubwa ni mbu wa kike .

Kwa mujibu wa Assenga, hatari kubwa ya mbu ilichukua nafasi pale walipoibuka aina mbalimbali ya wadudu wasioonekana (parasitic micro-organisms) ambao ndio wanaosababisha magonjwa yanayoenezwa na mbu hao tajwa.

Hapo ndipo anapotoa orodha ndefu ya mifano, kama vile mbu anayesababisha malaria anayejulikana kwa jina Plasmodium, pia wako wanaosababisha magonjwa hatari kama vile zika, dengue na homa ya manjano.

Assenga anarejea chanzo cha plasmodium, kwamba walitokana na wanyama jamii ya sokwe na mbu alipowauma wanyama hao, akabeba viumbe hao na kisha akimuuma tena mwanadamu na ndio ukawa mwanzo wa malaria kuenea.

Inaelezwa, ugonjwa malaria una athari na hatari kubwa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Wajawazito na watu wenye kasoro za kiafya, kinga yao iko chini huku takwimu za afya kimataifa zilionyesha inaua kwa kiwango kikubwa, hasa ukanda wa Bara Asia na Amerika ya Kusini.

Pia, kuna maradhi ya mabusha na matende, ambayo nayo ni mazao yanayoenezwa na mbu na kugharimu afya, maisha na uchumi wa wengi duniani.

**TAHADHARI ZILIZOPO**

Je, ni hatua gani zinazochukuliwa? Assenga anasema kuna tahadhari nyingi kitaifa na kimataifa, zinazopaswa au zilikwishachukuliwa ama kiserikali au kupitia asasi binafsi na mtu mmoja mmoja.

Anataja njia mojawapo ya kukabiliana na magonjwa, ni kwa kudhibiti mbu inayopendekezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), matumizi ya vyandarua vyenye dawa, huku mtaalamu huyo akikiri kushuhudia mwitikio chanya wa matumzi ya vidhibiti mbu hivyo.

Anarejea mtazamo wa jumla uliopo kwamba, kuna watu waliojitahidi kuitikia mwito, wakitumia vyandarua vyenye dawa na matokeo yanjionyesha ni kwamba, kiwango cha umma kuugua malaria kimepungua sana.

Hata hivyo, kila mafanikio yana kasoro zake, kwani kuna upande mwingine, wapo walioenda kinyume na mpango kama vile kuhujumu nyenzo kwa matukio kama ya vyandarua, kuhamishiwa matumizi mengineyo.

Kuna wakati ilitangazwa vidhibiti mbu kutumika katika kazi za uvuvi, jambo ambalo serikali ililazimika kuamua kuchukua hatua kukabili.

**MALAZI YA MBU**

Assenga anaeleza mazalia ya mbu ni maji ya aina mbalimbali yaliyotuama katika baadhi ya sehemu ambazo mbu wanatumia kutaga mayai.

Mbu aenezae malaria anaelezwa mazalia yake, ni pamoja na madimbwi mbalimbali ya maji kama yaliyoko kwenye maoteo ya mpunga yatokanayo na mafuriko, maji yaliyochepuka miferejini, kando ya mito na baada ya mito kupungua maji.

Pia, anataja maji yaliyotuama kando ya maziwa yanapopungua maji, mabwawa na mazingira mengine yanayofanana hali hiyo.

Assenga anaeleza kwa mbu aenezaye homa ya dengue na zika, mazalia yake kwa kiasi kikubwa ni magurudumu chakavu yaliyozagaa katika miji, chupa za maji, ndoo, majaba na vyungu vinavyohifadhi maji.

“Kila mmoja wetu anapaswa kuhakikisha mazingira aliyopo hakuna mazalia ya mbu, kwa kufukia madimbwi yenye maji au kutokuruhusu maji yasituame kwenye mazingra yetu,” anasema.

**CHANGAMOTO**

Assenga anasema, changamoto iliyoko ndani ya jamii ni kwamba kuna wengi wanaotilia maanani kwa kuchukua tahadhari binafsi za kuzuia uwepo wa mazalia ya mbu.

“Mara nyingi utakuta kwenye mazingira yetu kuna madimbwi na maji yaliyotuama na watu wanayaacha na hawaoni kuwa ni hatari,” anasema na kuendelea:

“Majumbani mwetu utakuta vyombo kama ndoo zenye maji, majaba, vyungu na vyombo vingine vyenye uwezo wa kuhifadhi maji vikiwa wazi na watu hawaoni kuwa ni hatari.

“Inawezekana ni kwa sababu jamii yetu haina elimu juu ya mazalia ya mbu au inafahamu, ila imepuuzia.

Watu wanashauriwa kuvaa nguo zenye kufunika sehemu kubwa ya mwili, ikiwa pamoja na mikononi na miguuni.

“Hizi ni pamoja na ‘tisheti’ na shati zenye mikono mirefu na suruali. Ikiwa mtu atashindwa kufanya hivi, basi anashauriwa kujipaka mafuta au ‘losheni’ yenye uwezo wa kufukuza mbu pindi awapo sehemu ambayo ina mbu.

“Hii yote itamsaidia mtu asiumwe na mbu na hivyo kupunguza au kuzuia kabisa uwezekano wa yeye kuambukizwa magonjwa yaenezwayo na mbu.”

Mtaalamu huyo anawasilisha kilio chake kwa serikali kupitia halmashauri zake mbalimbali nchini, kusimamia vita vya kutokomeza mazalia ya mbu, kuanzia ngazi za vitongoji, vijiji na wilaya nzima,

Anakumbusha kuwa dawa za kuua viluilui zitumike ipasavyo kutokomeza mazalia korofi ambayo ni pagumu ama kufunikwa au kuondolewa maji.

Asenga ansema, hadi sasa kuna nchi zilizokwishafanikiwa kutokomeza malaria, huku miaka ya nyuma kuna nchi anayotolea mfano kama Palestina na Italia zilifanikiwa kutokomeza malaria kwa kuwa na kampeni za nchi nzima za kutokomeza malaria haswa kutokomeza mazalio ya mbu. Ikiwa wao waliweza hata sisi tunaweza.

AFYA

## MAGEUZI MUHIMBILI

# Kauli za mashuhuda walioondolewa mawe tumboni bila kufanya upasuaji

- Kazi dakika 50, waendelea na safari
- Aliyetaabika miaka 7, apona saa 24

**Na Mary Geofrey**

SAMSON Makorere, mkazi wa Kinondoni jijini Dar es Salaam, ana maelezo ya kina kuhusu simulizi zilizomkaa na sasa historia kuhusu alivyoteseka kuugua maambukizi ya uchafu katika mkojo (UTI).

Ni adha na mateso ya miaka minane pasipo kugundua mzizi wa tatizo, hadi ghafla kupatikana majibu ya mahali ukweli ulikojificha.

Maisha hayo ya maradhi

Makorere anasimulia alidumu akitumia vidonge vya kuzuia maumivu makali, yaliyomkabili katika kipindi chote cha mateso, kabla ya shida ilikuwa mawe kwenye figo.

Anasimulia mwanzo wa mageuzi ni alipoenda hospitalini kufanyiwa uchunguzi na ndipo ilipogundulika kuwapo mawe kwenye figo la kulia, ikisababisha shida ya UTI sugu kwa miaka hiyo yote.

Anasema, alichukua hatua kwenda kupata matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), alikoambiwa ulazima wa kufanyiwa upasuaji wa kuyaondoa mawe hayo.

“Nilionana na daktari bingwa wa figo MNH, aliyenishauri nifanyiwe kipimo cha ‘CT-Scan’ kwa ajili ya kufahamu kwa kina tatizo na ndipo nilikutwa na mawe kwenye figo yangu ya kulia na kwenye mrija wa mkojo,”

Anaeleza alipangiwa daktari kufanyiwa upasuaji na alifanikiwa upande wa mrija wa mkojo walikoondoa jiwe la kwanza, ili kuokoa figo lingine lisipate madhara.

“Nilishauriwa nifanye upasuaji wa kuondoa jiwe kwenye njia ya mkojo kwanza, wakati nikijipanga kuondoa yaliyo kwenye figo. Lakini, baada ya upasuaji niliendelea kupata maumivu makali kwenye upande wa kulia wa figo ambao ulikuwa na jiwe la ukubwa wa sentimita 1.4,” anaeleza Makorere.

Ni kipindi alichokabili uhalisia kwa kutumia dawa za kupunguza maumivu wakati alipotafuta fedha za kumrejesha hospitalini, kutoa mawe kwenye upande figo la kulia.

Anasema wakati anasubiri, ndipo alipata taarifa kwamba Muhimbili Hospitali inaanzisha huduma ya kusaga mawe kwenye figo kwa kutumia nishati, pasipo upasuaji.

“Huduma ilipoanza kutolewa tu nilipigiwa simu na kuambiwa nije Mloganzila, ambako walisaga mawe yaliyokuwa kwenye figo kwa muda wa dakika 50 hadi saa moja, tena bila ya kusikia maumivu,” anaeleza Makorere.

Anafafanua, mara baada ya huduma hiyo, alimudu kwenda benki kuchukua fedha na akarejea, akisimulia: “Nilifanya malipo na kurejea nyumbani mwenyewe nikiwa mzima kabisa na hata huwezi kufahamu kama nimetoka hospitali na kuanzia pale sijawahi kusikia maumivu tena.”

Anaeleza, akiwa nyumbani alikunywa maji mengi kama alivyoelezwa alishuhudia ghafla mabadiliko, chembe za mawe zilianza kutoka kwa njia ya mkojo.

“Kama unavyoona haya mawe yametoka kwa njia ya mkojo yote kama mchanga au chembe chembe za mawe. Wakati yanatoka sikusikia isipokuwa kipande hiki kimoja kikubwa wakati kinatoka ndipo nilisikia maumivu makali,” anasema Makorere.



Samson Makorere, akifafanua jambo alipotoa ushuhuda. **PICHA ZOTE: MARY GEOFREY.**

**SHUHUDA MWINGINE**

Mwajuma Mbangwi, mkazi wa Kipunguni B, jijini Dar es Salaam, ana simulizi yake namna alivyosikia maumivu makali chini ya mbavu.

Hilo analieleza lilimfanya achukue hatua kwenda hospitali, ambako alibainika kusumbuliwa na ‘UTI’ na aliendelea kutumia dawa muda mrefu.

Anasema baada ya kutaabika na maumivu yasiyokoma, ni hali iliyomfanya apatiwe kipimo akaonekana na mawe kwenye figo.

“Nililazimika kwenda MNH ambako walinifanyia tema kipimo cha ‘CT-Scan’ na kuonekana nina mawe kwenye Figo nikapewa dawa za kunywa kama maji ambayo inasaidia kusaga mawe, lakini nilitumia tangu mwaka 2014 bila mafanikio,” anasema Mwajuma.

Anaeleza, alilazimika kurudi tena hospitali na baada ya uchunguzi, ilibainika jiwe kubwa lililobaki na akatakiwa kufanyiwa upasuaji na hata alipofanyiwa tena, maumivu makali hayakukoma.

“Nilirudi tena hospitali, wakaniambia nifanyiwe tena kipimo cha ‘CT-Scan’ na nilionekana bado jiwe lipo lilikuwa limejibanza kwenye mrija.

“Hivyo, nilipaswa kufanyiwa tena upasuaji, lakini walinishauri nisubiri kwanza kwa kuwa kuna huduma itaanzishwa na kusaga mawe kwenye figo,” anaeleza Mwajuma

Shuhuda huyo anasema, huduma hiyo mpya ilipoanza, Hospitalii Mloganzila walimpigia simu alikopatiwa huduma ya kusaga mawe kwa muda anaobashiri dakika 50 na akaruhusiwa kurudi nyumbani.

“Daktari alinishauri ninywe maji mengi na nining’inize miguu juu, ili mawe yaliyosagwa yatoke na wakati wa kupata haja ndogo nikojoe kwenye chombo, nichuje kuona kama yameanza kutoka.”

**MKURUGENZI MUHIMBILI**

Hospitali ya MNH, tawi la Mloganzila imeanza kutoa ya kuvunja mawe kwenye figo na mfumo wa mkojo kwa pasipo upasuaji ikitumia mawimbi mshituko.



Samson Makorere, akionyesha mawe yaliyotoka kwenye figo lake, kwa waandishi wa habari (hawapo pichani).

Inafanyika mara ya kwanza nchini, ikitumika mashine mpya na ya kisasa, inayotoa mawimbi yanayosafiri kupitia ngozi hadi iliyoko figo lenye jiwe au mawe na kuyavunja.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Museru, anasema mawimbi hayo hugeuka nishati inayovunja mawe madogo mithili ya mchanga na kutoka kwa njia ya mkojo.

Anasema ni teknolojia mpya na ya kisasa, inayoendeshwa na wataalamu tisa wazawa wa Muhimbili, waliopata mafunzo kwa njia ya mtandao wa ‘zoom’ kutoka kwa wenzao wa Korea.

Prof. Museru, anasema ni huduma iliyoanza mwanzoni mwa mwezi huu na zaidi ya wagonjwa 10 wameshanufaika na hali zao ni nzuri.

Anataja faida ya matibabu hayo, mgonjwa hahitaji kulazwa, hali inayosaidia kupunguza gharama walizotozwa zamani kufuata huduma nje ya nchi kwa Sh. milioni 10, sasa ni Sh. 500,000 na serikali hadi sasa imeshaokoa zaidi ya Sh. milioni 95

Kwa mujibu wa mchanganuo uliopo, mgonjwa wa rufaa anatozwa Sh. 500,000, binafsi Sh. milioni 1.2 na watokao nje ya nchi, Sh. milioni 4.8.

Prof. Museru anaeleza mwaka jana, jumla ya wagonjwa 1,035 wenye mawe kwenye figo walihudumiwa katika kliniki za nje ya Muhimbili, kati yao wapya 425, kati yao walilazwa 14 na kuna 50 waliofanyiwa upasuaji.

Aidha, kipindi cha mwaka 2010 hadi 2017, kuna wagonjwa 23 wenye matatizo hayo walipatiwa rufaa kwenda nje ya nchi.

**DALILI ZAKE**

Tabibu Bingwa wa Magonjwa ya Mfumo wa Mkojo, Dk. Isack Maro, anataja dalili zake ni maumivu chini ya mbavu na kuna wakati mgonjwa anakojoa damu, kama jiwe alilo nalo ni kubwa na limekwangua ukuta wa figo.

Anasema, pia mgonjwa anaweza kupata maumivu makali abapokojoa iwapo kuna jiwe lililopata maambukizi ya bakteria, hata kukojoa usaha na mkwamo wa mkojo kwa mwenye tezi dume.

Bingwa huyo anafafanua , awali walipofanya upasuaji ilimchukua mgonjwa wastani wa mwezi mmoja hadi mitatu kupona, lakini matibabu mapya hayazidi wiki.

Chanzo kikuu anakieleza ulaji wa ziada vyakula kama nyama nyekundu; mkojo unapokuwa na kemikali na madini mengi, pale mtu hanywi maji ya kutosha, pia mabadiliko ya hali ya hewa kwa baadhi ya maeneo.

MAZINGIRA

# Uvamizi kuni za kupikia msituni unavyoitafuna Hifadhi ya Jozani

- Angalizo: Nusu iko mbioni kutoweka
- Suluhisho la gesi haijafikishwa vijijini
- Umeme uliowafikia, kote hawaupikii

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

ATENDEA Mkanga (35), anatamani kila siku kutumia gesi kwa ajili ya kupikia, lakini anashindwa kutokana kutokuwepo kijijini kwao, hivyo anajikuta akiendelea kutumia kuni na mkaa.

Mama huyo mwenye familia ya watoto watatu anaishi katika kijiji cha Charawe, mkoa wa Kusini Unguja. Anatumia shilingi 25,000 kila mwezi kwa ajili ya kununua kuni anazotumia kupikia chakula kwa ajili ya familia yake.

Charawe ni miongoni mwa vijiji tisa, vilivyomo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Jozani, ambayo kwa kiasi kikubwa imeathiriwa na uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji miti ya asili, licha ya kuwa ni kivutio kikubwa cha utalii.

Kijiji anachoishi Atendae, kina wakazi 1,539 wanaoumudu kununua gesi, lakini wanaikosa kwa sababu ya kutokuwepo biashara hiyo kijijini hapo na kwa jumla, wakazi walioko ni kaya 480 ambazo zote zinatumia nishati za kuni na mkaa pekee kupikia.

"Duka la kuuza gesi lipo Jozani, ambako ni umbali kilomita zaidi ya 20 kutoka hapa. Pia, hakuna usafiri wa gari, usafiri pekee uliopo ni baiskeli na bodaboda ambayo kuikodi ni shilingi 5, 000," anasema mama huyo.

Atendae anasema, wafanyabiashara wengi katika sekta ya gesi wamewekeza maeneo ya mjini na vijiji ambavyo ni maarufu kwa biashara ya utalii.

Kwa hiyo, licha ya kupenda kutumia nishati gesi, kwa imani ni rahisi, hasa ikizingatiwa upatikanaji wa kuni umekuwa mgumu, hata kuwafanya wakazi hao watumia nguvu na muda mrefu kuzipata.

"Hivi sasa serikali inapinga marufuku ukataji miti na kijiji chetu kimezungukwa na Mbuga (Hifadhi) ya Taifa ya Jozani, hivyo ni vigumu kupata kuni kwa ajili ya kupikia," anasema.

Mkazi mwingine, Fatma Mahmoud (40), anasema licha ya gesi kukosekana, pia hata suala la uelewa kuhusu matumizi salama ya nishati hiyo hakuna.

"Tukishapewa elimu juu ya matumizi ya gesi, tutaondoa hofu na tutakuwa na ari kubwa ya kuitumia," anasema, huku akiunga hoja ya mtangulizi kwamba, kukosekana gesi, kufanya wanawake wanaendelea kuumia.



Rehema Shauri, mkazi wa Kijiji cha Ukongoroni, Mkoa wa kusini Unguja, akipika kwa kutumia kuni nyumbani kwake. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

> **"Tumefika wakati sasa kuhakikisha tunabadili mwelekeo wetu, tuko kwenye mkwamo na hatuna jinsi zaidi ya kuhamasisha wanavijiji kutumia gesi," alisema.**

Anasema, imefika hatua wanalazimika kuamka alfajiri kwenda msituni kutafuta kuni, hivyo inawakosesha fursa nyinginezo za maendeleo.

Hadi sasa inaelezwa, matumizi ya kuni na mkaa yanazidi kuangamiza misitu ya Zanzibar na ripoti uliouopo sasa kuhusu Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka Zanzibar, inasema kila mwaka kuna ekari 100 za miti zinapotea.

Haroub Abdi Abdallah (39), ni baba mwenye watoto watano. Ana maelezo kuwa, matumizi ya kuni ya yanaharibu mazingira, pia kubadilisha rangi ya nyumba zao.

"Tunahitaji sana gesi, kwa sababu kuni zinachafua nyumba zetu hivyo inatulazimu kila mwaka kubadilisha rangi ili kuwa na mwonekano mzuri," anasema.

Haroub, anakiri shida ya upatikanaji kuni hivi sasa umepungua tofauti na miaka 10 iliyopita, kutokana na ongezeko la wakazi wake.

### UMEME UPO, HAUPIKIWI

Inaelezwa tatizo hilo la kukosekana gesi na shida ya kuni, pia lipo katika kijiji jirani cha Ukongoroni, ambacho kina kaya 240 na huduma za umeme zilizounganishwa kutoka gridi ya taifa kwa wakazi 850, lakini hautumiwi kupikia.

Mkazi wa kijijini hapo, Usheza Mwita Makame (60), anasema wanatumia kuni na mkaa, kwa sababu ndio inayopatikana kIrahisi kwao.

Usheza, ana angalizo kwamba, kuendelea kutumia kunaathiri mazingira ya Hifadhi Jozani, inapunguza idadi ya miti ya asili, wanayotumia kwa ajili ya tiba asili.

"Zamani mtu akiumwa na ugonjwa wa pumu tulikuwa tunaingia msitu kutafuta magome ya Myuwi pumu inapoa, lakini sasa umetoweka kabisa kwa sababu ya ukataji wa miti," anasema.

Mamlaka zinaeleza kuwa ukataji miti umezidi kuangamiza misitu na sasa wakazi hao wameanza kuvamia eneo la hifadhi.

### HOFU INAYOTAWALA

Msaidizi wa kiongozi wa serikali ya kijiji hicho, Fadhil Sudi Mlenge (40), anasema, licha ya mamlaka ya kiserikali kutenga eneo maalum kwa wanakijiji kukata kuni, sasa hivi eneo limepungua kutokana na kuongezeka matumizi na wanakijiji wanavamia hifadhini.

"Muda wa kutumia gesi umefika, wanakijiji wanaihitaji lakini changamoto ni jinsi ya kuipata. Hivyo, tunawaomba wafanyabiashara wasogeze huduma hii kijijini kwetu," anasema kiongozi huyo wa serikali.

Awesu Shabani Ramadhani, Naibu Katibu wa Jumuiya ya Hifadhi ya Mazingira Jozani (JECA), inayonufaika na mgawo wa mapato yanayotokana na watalii wanaotembelea msitu huo, sasa ana hofu kutakuwapo athari zaidi, kama hatua hazitachukuliwa.

Ubashiri wake ni kwamba, pasipochukuliwa hatua za udhibiti katika miaka 20 ijayo, kuna uwezekano nusu ya msitu huo unaoingiza mapato zaidi ya Sh. bilioni 1.3 kwa mwaka, utakuwa umeathirika.

"Mbuga ya Taifa ya Jozani ndio roho ya uchumi wa wa vijiji tisa vilivyomo katika msitu huu, vikiwamo Charawe na Ukongoroni, hivyo kama juhudi za kudhibiti uharibifu hazitachukuliwa, litakuwa pigo kubwa kwa wanavijiji.

"Hivi sasa, tuhamasishe shughuli za uzalishaji mali ambazo haziharibu misitu, ikiwamo kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia umeme wa jua kwa ajili ya ili kuhakikisha wanavijiji wanakuwa na kazi mbadala na kuachana na uharibifu wa misitu," anasema.

Awesu anasema, miti ya asili kama mikoko inayozuia maji ya bahari kuvamia vijiji na maeneo ya kilimo, ndio inayokatwa kwa wingi kwa ajili ya kuzalisha mkaa, kwa sababu wanavijiji wanaamini una mkaa mzuri.

### OFISA MISITU

Rahika Hamad Suleiman, Ofisa kutoka Kitengo cha Elimu ya Misitu kwa Wanajamii katika Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka Zanzibar, anasema asilimia 65 ya wananchi Zanzibar na wanavijiji tisa kati ya 10, wanatumia kuni na mkaa kupikia.

Anasema ni hali inayosababisha baadhi ya wanyama kama Chui waliopatikana Zanzibar kwa muda mrefu, sasa wanatoweka, baada ya kushambuliwa na wanavijiji.

Pia, anawataja wanyama kama Paa Nunga na Kima Punju, ambao ni kivutio kikubwa cha utalii, wameanza kuadimika.

Anasema, pia vianzio vya maji kama mabwawa yaliyokuwa yakipatikana katika Hifadhi ya Taifa ya Jozani, ambayo yalitumiwa na wanyama kunywa maji, yamekauka baada ya watu kukata miti.

"Tumefika wakati sasa kuhakikisha tunabadili mwelekeo wetu, tuko kwenye mkwamo na hatuna jinsi zaidi ya kuhamasisha wanavijiji kutumia gesi," alisema.

Ofisa huyo anasema, Idara ya Misitu inaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu matumizi ya gesi na majiko sanifu yanayotumia kiwango kidogo cha kuni, ili kulinda mazingira yaliyopo.

Pia anasema wauza gesi visiwani wanakiri kutofikia katika sehemu kubwa ya vijiji, kutokana na uhaba wa gesi inayoingizwa nchini.

Msambazaji wa gesi V-Gas Zanzibar, Taufiq Salum, anasema bado hawajayafikia masoko mengi ya vijijini, kutokana na uhaba wa bidhaa hiyo inayoingizwa visiwani, kwani kuna upungufu wa miundombinu ya kuhifadhi.

Anaahidi changamoto hiyo itaondoka karibuni, baada ya ujenzi wa bandari ya kupakua gesi inayojengwa Mangapwani, Unguja kukamilika.



## HABARI DODOMA

# Wizara yasaini mkataba kukabili sumukuvu

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WIZARA ya Kilimo imesaini mkataba wa ujenzi wa vihenge vya kuhifadhia mazao ya mahindi na karanga ili kukabiliana na tatizo la sumukuvu.

Ujenzi huo utafanywa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO).

Akizungumza baada ya kusaini, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Gerald Kusaya, alisema ujenzi huo utafanyika kwenye halmashauri 20 za Tanzania Bara na maeneo mawili ya Tanzania Visiwani.

Alisema ujenzi huo umetokana na kutohifadhi vizuri chakula hasa mazao ya karanga na mahindi na hivyo kupatwa na sumukuvu.

Kusaya alisema serikali imetoa Sh. bilioni 3.8 zitakazopelekwa SIDO ili kusaidia kutoa mafunzo ya ujenzi wa vihenge.

"Nitafuatilia fedha hizi ili kuona zinatumika vizuri kwa malengo yaliyokusudiwa ili kuondokana na tatizo la sumu kuvu," alisema.

Aliwataka watendaji wakuu wa SIDO kutimiza wajibu wao katika suala hilo kwa kuwa fedha hizo ni za umma zionyeshe matokeo chanya.

Alitoa wito kwa wananchi kuwa miradi itakapokamilika waitunze ili iwasaidie kwa kuwa tatizo la sumukuvu ni kubwa.

"Katika kutekeleza mradi huu wizara itashirikiana na taasisi nyingi kama SIDO, VETA, TPRI, TARI, CPB, TBS na taasisi nyingine ambazo zinahusiana na masuala ya chakula, ni jukumu letu sisi wizara kuhakikisha hii mipango tunayopanga inakamilika kwa wakati," alisema.

Alisema wizara hiyo inatarajia kusaini mkataba na makandarasi ambao wataenda kujenga maabara na kituo mahiri cha usimamizi wa mazao ya nafaka.

Mkurugenzi wa SIDO, Prof. Sylvester Mpanduji, alisema shirika linatoa teknolojia, mafunzo, mikopo na kuhamasisha utafutaji wa masoko.

Naye, Mratibu wa Mradi wa sumukuvu, Clepin Mbekomize, alisema VETA inatarajia kutoa mafunzo kwa vijana 400 ya teknolojia ya kutengeneza vihenge.

**"Katika kutekeleza mradi huu wizara itashirikiana na taasisi nyingi kama SIDO, VETA, TPRI, TARI, CPB, TBS na taasisi nyingine ambazo zinahusiana na masuala ya chakula, ni jukumu letu sisi wizara kuhakikisha hii mipango tunayopanga inakamilika kwa wakati," alisema.**

# Walimu watakiwa kuandaa mazingira rafiki shuleni

**Na Ibrahim Joseph, BAHI**

MKUU wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, amewaagiza wakuu wa shule na walimu wakuu kuandaa mazingira rafiki kwa kuzingatia mwongozo wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili kuwalinda wanafunzi na maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Agizo hilo alilitoa jana alipokuwa akizungumza kwenye kikao kazi na wakuu wa shule cha kuweka mikakati ya maandalizi kabla ya kufunguliwa Juni 29, mwaka huu.

Alisema viongozi hao wanapaswa kuweka mazingira kulingana na matakwa ya mwongozo huo kabla ya shule kufunguliwa.

"Tunajua tunaenda kufungua shule wiki ijayo hakikisheni mnaandaa mazingira mazuri ya kuwatunza wanafunzi watakapoingia na kutoka shuleni ili kujikinga na ugonjwa wa corona," alisema.

Alizitaka shule kuandaa vifaa vya kutosha vya kutakasa mikono.

Aliwataka walimu wa masomo yote kujipanga vizuri ili kuhakikisha wanafundisha kwa bidii na kumaliza mihula ya masomo.

"Viongozi wenzangu ili tuinue kiwango cha ufaulu na kuboresha sekta ya elimu katika wilaya yetu ni lazima tutimize wajibu wetu wa kufundisha kwa bidii huku tukidumisha upendo na kushirikiana kwa pamoja kutatua changamoto zinazojitokeza mbele yetu," alisema.

"Walimu twendeni tukalishinde jaribu hili lililoikumba wilaya yetu na taifa letu kwa kuchapa kazi ipasavyo kwa kuwa muda ni mchache na watoto wetu wamekaa nyumbani kwa muda mrefu bila kufundishwa, tuwasaidie ili wafaulu vizuri."

Kwa upande wake, Ofisa Elimu Sekondari wilayani hapo, Helen Mselemu, alisema walimu wamejiandaa na wameitumia likizo yao kuandaa masomo.

Hata hivyo, alisema kutokana na mazingira ya vijiji wanafunzi walilazimika kuyafuata shuleni hapo kwa ajili ya kwenda kujisomea nyumbani.

Ofisa elimu msingi wa wilaya hiyo, Mohamed Msongo, aliahidi kufanyakazi kwa bidii ili kuhakikisha ufaulu wa wanafunzi unaongezeka wilayani hapo.

Alisema katika mtihani wa darasa la saba mwaka 2019 wilaya hiyo ilishika nafasi ya tatu kimkoa na wamejipanga kwa mwaka huu kushika nafasi ya kwanza.




Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo (kushoto), akipokea sehemu ya viti 75 na meza 45 kutoka kwa Mkurungenzi wa Taasisi ya Dk. Msuya, Dk. Ombeni Msuya (kulia), zilizofanyiwa ukarabati kwa thamani ya zaidi ya Sh. milioni moja, kwa ajili ya shule ya sekondari Ibihwa, wilayani Bahi, mkoani Dodoma, jana. Wapili kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# NIRC yakabiliwa uhaba fedha kutekeleza shughuli zake

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

TUME ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC), inakabiliwa na uhaba wa fedha za kutekeleza shughuli zake, kutokana na kupatiwa ukomo mdogo wa fedha ikilinganishwa na mahitaji halisi.

Hayo yalielezwa hivi karibuni na Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, Daudi Kaali, katika taarifa yake ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali, kwa Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, jijini Dodoma.

Alisema pamoja na rasilimali fedha ndogo inayotengwa kwa sekta ya umwagiliaji, fedha zinazoidhinishwa na Bunge hazitoki kwa wakati kwa mtiririko unaotakiwa na wakati mwingine hazitoki kabisa.

Alifafanua kuwa kuanzia mwa mwaka 2014/15 hadi 2019/20, fedha za ndani zilizoidhinishwa ni Sh. bilioni 41.6 na zilizotolewa ni Sh. bilioni 3.77.

"Kwa upande wa fedha za nje kwa kipindi hicho kiasi cha Sh. bilioni 159.5 kiliidhinishwa na zilizotolewa ni Sh. bilioni 29.3," alisema.

Alisema athari za mabadiliko ya tabia nchi zilijidhihirisha kwa uharibifu wa miundombinu ya umwagiliaji unaosababishwa na mafuriko na kupungua kwa tija ya uzalishaji kutokana na ukame.

Vilevile, alisema vyanzo vya maji vimekauka kutokana na uharibifu wa mazingira na katika msimu wa kilimo mwaka 2019/20, Tume imeainisha jumla ya skimu 40, zilizopata athari ya mafuriko, yaliyotokana na mvua za vuli na masika.

"Tume inaendelea kufanya tathmini ya uharibifu na athari za mafuriko katika skimu za umwagiliaji ili kujua gharama za ukarabati wa skimu hizo," alisema.

Pia, alisema katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa vyanzo vya maji, Tume itaendelea kujenga mabwawa madogo, ya kati na makubwa kwa ajili ya kuhifadhi maji ya umwagiliaji.

Alisema wanaendelea kuhamasisha na kuendeleza matumizi ya teknolojia za umwagiliaji zinazotumia maji kwa ufanisi.

"Pia kuhamasisha, utunzaji wa vyanzo vya maji na mazingira kwa kushirikiana na mamlaka husika kulingana na sheria na kanuni zilizowekwa," alisema.

Alisema pia Tume inakabiliwa na uhaba wa wataalamu wa umwagiliaji na ina ofisi ya umwagiliaji makao makuu, mikoa na wilaya.

Alisema, ili kutimiza takwa la kisheria la kuwa na ofisi ya umwagiliaji kila mkoa na wilaya katika kuimarisha usimamizi wa skimu za umwagiliaji, inatakiwa kuwa na wataalamu 438 wa fani mbalimbali katika ngazi zote.

"Kwa sasa Tume ina watumishi jumla 213, tu wakati mahitaji halisi ni kuwa na watumishi 438, hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 225," alisema.





# Tanzania ina upungufu wa ngano tani 900,000

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

TANZANIA inakabiliwa na uhaba wa tani 900,000 za ngano kwa mwaka, hali ambayo inailazimu serikali kutumia fedha nyingi za kigeni kuagiza zao hilo kutoka nje ya nchi ili kukidhi mahitaji ya taifa.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Lugendo Bucheyeki, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema uzalishaji wa ngano nchini ni tani 100,000 tu kwa mwaka wakati mahitaji ya zao hilo kwa Watanzania ni zaidi ya tani 1,000,000, hivyo kuna uhaba wa tani zaidi ya 900,000 zinazohitajika kila mwaka ili kukidhi mahitaji ya Watanzania.

Alisema kwa sasa nchini ngano inalimwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kaskazini pekee, na kwamba ili kupunguza tatizo la uhaba wa ngano, upo umuhimu wa kuhamasisha maeneo mengi zaidi kulima zao hilo.

Alisema TARI imefanya utafiti na kubaini yapo maeneo mengine ambayo yanaweza kulima ngano nchini ingawa wananchi wanaoishi maeneo hayo wanahitaji ushauri wa kitaalaamu ili kujikita katika kilimo cha ngano.

"Ili kukidhi mahitaji ya ngano nchini, ni lazima tupanue maeneo ya kilimo cha zao hili, sisi TARI tumeshafanya utafiti na kubaini maeneo ambayo yanaweza kulima ngano na tunajiandaa kutoa ushauri wa kitaalamu ili wananchi waweze kulima zao hilo," alisema Bucheyeki.

Alisema TARI pia imefanya utafiti wa mbegu bora za ngano ambazo zinaweza kuvumilia hali ya hewa na kutoa mavuno mazuri katika maeneo ambayo hayalimi zao hilo.

Mmoja wa wafanyabiashara wa ngano katika Soko la SIDO, Blanka Chaula, alisema kutokana na uhaba wa zao hilo shambani ambalo awali walikuwa wananunua shilingi 20,000 kwa plastiki moja, kwa sasa wananunua shilingi 28,000.

Alisema kuadimika kwa ngano kunasababisha na wafanyabiashara kuuza kilo moja ya ngano shilingi 1,300 kutoka 1,000 ya awali.

Katika kikao chake na wadau wa kilimo kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ya Mbeya, Songwe na Katavi, Ofisa Kilimo Mkuu kutoka Wizara ya Kilimo, Idara ya Maendeleo ya Mazao, Melyus Zalawahe, alisema serikali imejipanga kuhakikisha zao hilo linalimwa kwa wingi nchini.

Alisema licha ya mikoa kama Manyara na Mbeya kuzalisha kwa wingi zao hilo, lakini wanaendelea na mikakati ya kuhakikisha wanaendelea kulima ngano kwa tija.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (katikati), akiwapongeza viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, jana, baada ya kukamilisha ujenzi wa Zahanati ya Garijembe ambayo imejengwa mahususi kwa ajili ya kutoa huduma za afya kwa wanafunzi wa shule ya sekondari ya wasichana ya vipaji maalum ya Garijembe kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 70. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mil. 500/- kupanua kituo cha afya kuwa hospitali ya wilaya

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

SERIKALI imetoa kiasi cha fedha shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuongeza majengo kwenye Kituo cha Afya cha Igawilo kilichopo katika Bonde la Uyole jijini Mbeya kwa lengo la kukipandisha hadhi kuwa hospitali ya wilaya.

Akizungumza na wakazi wa Kata ya Igawilo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema fedha hizo zilitolewa kupanua Kituo cha Afya ili kipandishwe hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya.

Alisema ujenzi umeanza kwa ajili ya kukarabati na kuongeza majengo mengine muhimu ya kutolea huduma na kwamba unatarajiwa kukamilika kabla ya Septemba mwaka huu.

"Serikali imeshaingiza fedha shilingi milioni 500 kwenye akaunti ya halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya, lengo letu tunakipandisha kiwe hadhi ya hospitaji ya jiji... tutahakikisha miundombinu yote ya kutolea huduma inakuwapo, tunasisitiza ujenzi huo ukamilike kwa wakati kufika Septemba mwaka huu," alisema Chalamila.

Baadhi ya wakazi wa Jiji la Mbeya walisema uamuzi wa serikali kukipandisha hadhi kituo hicho cha afya wameupokea kwa mikono miwili, wakiamini hospitali hiyo itakuwa ni msaada mkubwa kwa wakazi wa Bonde la Uyole na maeneo jirani.

Alisema wanaendelea kupata huduma kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya licha ya kutumia umbali mrefu, hivyo kukamilika kwa kituo hicho kutasaidia kupunguza gharama na muda kupata huduma za matibabu.

Flora Fumbo na wenzake, waliahidi kushirikiana na mafundi wanaojenga hospitali hiyo kuhakikisha kazi hiyo inakamilika haraka na hatimaye waweze kupata huduma bora za afya jirani na makazi yao.

## Mbarali walalamikia maji yasiyo salama

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

WAKAZI wa Kitongoji cha Mayota kilichopo Mamlaka ya Mji Mdogo Rujewa wilayani Mbarali, wamedai wanatumia maji yaliyochanganyika na udongo ambayo wanayapata kwenye visima kutokana na tatizo la maji kwenye eneo hilo.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa kitongoji hicho, Ezekiel Njugunya, wakati akizungumza na Nipashe juu ya tatizo la maji ambalo alisema limechangia kwa kiasi kikubwa kukwamisha shughuli za uzalishaji ikiwamo biashara za mamalishe.

Alisema tatizo la maji linatokana na kukosekana na maji ya mabomba na kuwalazimu wakazi wa eneo hilo kuchimba mifereji na visima vidogo, ambavyo hutoa maji yaliyochanganyikana na tope ambayo ni hatari kwa afya zao.

Alidai adha ya maji hutokea hasa kipindi hiki ambapo mvua zimekata, hivyo hakuna mahali pengine wanapata huduma ya maji zaidi ya kwenye visima.

"Wananchi wangu wanalazimika kunywa maji yaliyochanganyikana na tope hasa wakati wa kiangazi... tunaomba viongozi mtusaidie maana kila mara nimekuwa nikiwakumbusha tusaidiane ili kuwanusuru wakazi hawa tuwapatie huduma ya majisafi na salama," alisema Njugunya.


Tatizo la maji ya bomba limedumu kwa zaidi ya miaka 10, hali ambayo inasababisha wananchi kutumia muda mwingi kutafuta maji badala ya kufanya shughuli za uzalishaji mali.

Yazidu Abdul, mkazi wa Mtaa wa Kaniyonga, alisema licha ya kukosekana kwa huduma ya maji katika mtaa wake, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika mji huo (RUWASA), imekuwa ikiwatoza wananchi kiasi cha shilingi 5,000.

Alisema licha ya kutozwa kiasi hicho cha fedha, lakini hakuna huduma ya maji na kwamba kinamama wamekuwa wakitumia muda mwingi kutafuta maji badala ya kujikita kwenye shughuli za uzalishaji.

Kaimu Ofisa Mtendaji wa RUWASA, Tuntufye Chamba, alisema alilifikisha suala la uhaba wa maji kwa watendaji wa RUWASA ambao ndio wenye jukumu la kusimamia usambazaji wa maji.

Chamba alisema kitongoji cha Mayota ni miongoni mwa maeneo ya kimkakati kwa ajili ya kupelekewa huduma ya maji na kwamba wamepokea fedha kutoka kwa wafadhili kwa ajili ya kuchimba visima vya maji.





# Balozi Iddi awapa somo waanzisha miradi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Iddi, amewataka wananchi kuzingatia ushauri wa wataalamu wakati wanapoanzisha miradi ya maendeleo ili iweze kutoa huduma kwa ufanisi na kudumu kwa muda mrefu.

Alisema ipo baadhi ya miradi ya wananchi inayofifia na mingine kufa baada ya kukosa usimamizi wa kitaalamu jambo linaloleta usumbufu na hatimaye hukosa matumaini ya kuiendeleza.

Balozi Iddi alisema hayo alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya mradi wa majisafi na salama katika Kijiji cha Fujoni, unaendeshwa kwa nguvu za wananchi ambao tayari umeshafikia hatua ya ujenzi wa mnara wa kuhifadhia matangi ya maji baada ya kumalizika kwa uchimbaji wa kisima.

Aliwapongeza wananchi wa kijiji hicho kwa uamuzi wao wa kujitafutia maendeleo kwa jitihada zao wenyewe na kuondoa changamoto inayowakabili ya upatikanaji hafifu wa huduma za majisafi na salama katika kijiji chao.

Balozi Iddi ambaye pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Mahonda, aliwahakikishia wananchi hao kwamba hatochoka kuunga mkono juhudi zao kwa kutia nguvu zitakazoamsha ari ya kukamilika kwa wakati miradi ya kijamii hasa ile ya huduma za majisafi na salama.

Msimamizi wa mradi huo, Ali Omar Maulidi, alisema awamu ya kwanza ya uchimbaji wa kisima imeshafikia hatua nzuri na kwa wakati huu nguvu zao wamezielekeza kwenye ujenzi wa mnara wa kuhifadhi matangi wawili yenye ujazo wa lita 15,000.

Alisema kinachosubiriwa kwa sasa ni hatua ya kumwaga zege ili kukamilisha kazi hizo zitakazokwenda sambamba na miundombinu ya usambazaji wa mipira ya maji katika mitaa ya kijiji hicho.

Akitoa shukrani kwa niaba ya wananchi wa Kijiji cha Fujoni, mmoja wa wazee alimshukuru mwakilishi wao kwa moyo wa kuendelea kuunga mkono nguvu za wananchi licha ya kutangaza kutogombea tena uwakilishi kwenye uchaguzi wa mwaka huu.



Mwenyekiti wa Wawakilishi Wanawake Zanzibar (UWAWAZA), ambaye ni Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma, akitoa pongeza kwa mke wa Rais wa Zanzibar, Mwanamwema Shein (hayupo pichani), mjini Zanzibar jana, kwa ushirikiano alioutoa katika shughuli za maendeleo zikiwamo za kijamii. **PICHA: IKULU**

## UWAWAZA wampongeza mke Rais Shein

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

UMOJA wa Wawakilishi Wanawake katika Baraza la Wawakilishi (UWAWAZA), umempongeza mke wa Rais wa Zanzibar, Mwanamwema Shein kwa kushirikiana nao kikamilifu katika mapambano ya wanawake kuona wanapata haki zao za msingi.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake katika Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, alisema wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamefurahishwa na juhudi za mke wa rais ambaye katika kipindi cha miaka 10 alikuwa mstari wa mbele kutetea haki za wanawake na watoto kwa kutumia nafasi yake.

Mgeni ambaye ni Spika wa Baraza la Wawakilishi, alisema ushiriki wake katika kazi mbalimbali ikiwamo za huduma za jamii pamoja na masuala ya afya kwa kinamama, yamesaidia kutoa msukumo kupunguza vifo vya wajawazito kwa kujifungua vituo vya afya.

"Sisi Wawakilishi wa Umoja wa Wanawake wa (UWAWAZA) kwa kiasi kikubwa tumefurahishwa na juhudi zake mama Mwanamwema kwa sababu alikuwa na ushirikiano na sisi mkubwa katika matukio mbalimbali ambayo yalikuwa na lengo la kuimarisha huduma za wanawake na kupiga hatua ya maendeleo," alisema.

Alisema, mama Mwanamwema alishiriki vizuri katika chanjo ya watoto wanapozaliwa hadi miaka mitano na kusaidia kupunguza vifo na maradhi hatari yanayowashambulia watoto na kusababisha vifo ikiwamo kifaduro, pepo punda na surua.

UWAWAZA umemtakia kila la kheri mama Mwanamwema mapumziko yake pamoja na mumewe Dk. Ali Mohamed Shein kwa kumaliza muda wa urais wa miaka 10 kwa mujibu wa Katiba.

# TAMWA yawapa kongole wanawake watiania urais

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake, Tanzania (TAMWA), upande wa Zanzibar kimewapongeza watiania watatu wanawake waliothubutu kuchukua fomu ya kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar.

Watiania hao ambao ni makada wa CCM ni Mwantum Mussa Sultan na Hasna Attai Massoud na Fatma Kombo Masoud, ambao wanataka kumrithi Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema wanawake hao ni majasiri na wanafaa kuwekwa katika vitabu vya historia.

"Mwantum, Hasna na Fatma ni wanawake pekee hadi sasa waliojitokeza kwenye wanaume 23 wenye nia ya kuwania nafasi hiyo," alisema Dk. Mzuri.

Alisema mwaka 2000, Balozi Amina Salum Ali alikuwa mwanamke pekee aliyejitosa kugombea urais wa Zanzibar na pia mwaka 2015 alichukuwa fomu kugombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia CCM.

Dk. Mzuri alisema ili kufanikisha lengo la uwiano sawa wa wanawake katika vyombo vya maamuzi, TAMWA inapenda kuona ushiriki wa wanawake wengi zaidi wanajitokeza kuchukua fomu ya kugombea nafasi hiyo.

Alisema wakati wa uchukuaji fomu kwa nafasi ya urais ukiendelea, TAMWA Zanzibar inapenda kuwahamasisha wanawake kujitokeza na kutumia haki yao hiyo ya kikatiba na kidemokrasia.

"Ikumbukwe kuwa Zanzibar ina historia kubwa ya wanawake kushiriki katika mapambano ya kudai uhuru kwa namna mbalimbali ikiwamo kupinga kwa uwazi ukandamizaji dhidi ya wakoloni wakati wanaume wengi waliogopa," alisema.

Alisema kutokana na kukua kwa mfumo dume hivi sasa wanawake wanavunjwa moyo kugombea nafasi hizo pamoja na kuwa wao ndio walio wengi nchini zaidi ya asilimia 50 na ndio wanaokumbwa na changamoto zaidi zikiwamo za kiuchumi na kijamii.

Dk. Mzuri alisema, wanawake pia wamethibitika duniani kote pamoja na Zanzibar kuwa ni watu wanaopenda kujitolea, waaminifu na pia wanaopenda kufanya maamuzi kwa njia ya ushirikishi.

"TAMWA, Zanzibar inapenda kuwashauri wapenda maendeleo wote kuendelea kuwaunga mkono wanawake walioonyesha nia ya kugombea nafasi za uongozi ili waweze kushinda na hivyo kuleta usawa wa kijinsia katika nchi pamoja na usawa kwa ujumla," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI YA DEREVA NA MAUZO** Mwenye uzoefu wa kuuza Maji. PIga simu namba : **0767 269677 saa za kazi**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



115787802

**Limi Kiyumbi** anatangaza kupotea kwa cheti cha Kidato cha Nne chenye Index namba **S.1066-0005** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2014 katika Shule ya Sekondari Ntuzu . yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **LIN/LIN/RB/409166/2020**

## KUPOTEA KWA PASSPORT HATI YA KUSAFIRIA



115788202

**Witness Willy Bathromew** anatangaza kupotea kwa Passport / hati ya kusafiria yenye namba **TAE09635** 1iliyotolewa mwaka 2019 na Wizara ya Uhamiaji Dar es salaam. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/CE/RB/472250/2020**

## CHETI KIMEPOTEA



115788002

**EFESO RUBEN MGAYA** anatangaza kupotelewa na cheti cha Kidata cha nne chenye Index **No.S1157-0041** Kilichotolewa na **IWAWA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2006. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.taarifa ya polisi: **MBE/MBE/RB/458092/2020.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**RUFAA/MADAI NO.7/2020**

**Katika Mahakama wilaya ya Dodoma**

**Shauri La Rufaa Jinai/Madai No. 7/2020**

**Katika Mahakama ya Wilaya Dodoma**

**CRJE…………………………………Mrufani**

**Dhidi ya**

**BARIKI KAMOTA……………………Mrufaniwa**

**KWA : BARIKI KAMOTA.**

Kwa kuwa rufaa iliyotajwa hapo juu itasikilizwa katika Mahakama iliyotajwa hapo juu siku ya 15/7/2020

Unatakiwa uhudhurie katika Mahakama hiyo Mrufani Mrufaniwa Shahidi pamoja na vielelezovyovyote kama vipo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Mhuri wa Mahakama hii leo 29/5/2020.

115787902

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**RUFAA/MADAI NO.7/2020**

**Katika Mahakama wilaya ya Dodoma**

**Shauri La Rufaa Jinai/Madai No. 7/2020**

**Katika Mahakama ya Wilaya Dodoma**

**CRJE…………………………………Mrufani**

**Dhidi ya**

**Musa Kamota……………………………Mrufaniwa**

**KWA: MUSA KAMOTA.**

Kwa kuwa rufaa iliyotajwa hapo juu itasikilizwa katika Mahakama iliyotajwa hapo juu siku ya 15/7/2020

Unatakiwa uhudhurie katika Mahakama hiyo Mrufani Mrufaniwa Shahidi pamoja na vielelezovyovyote kama vipo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Mhuri wa Mahakama hii leo 29/5/2020

115787902

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Watoto mapacha watatu wazaliwa na ugonjwa corona

**MEXICO, Mexico**

MAPACHA watatu waliozaliwa hivi karibuni nchini Mexico wamekutwa na maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona, kikiwa ni kisa cha kwanza, kulingana na mamlaka ya afya.

Mapacha hao - walizaliwa kabla ya muda, Juni 17 huko Mexico na wote wakapatikana na virusi vya corona siku waliyozaliwa.

Wataalamu wa afya bado wanachunguza ikiwa watoto hao waliambukizwa kupitia kondo la nyuma la mama wakati wa ujauzito.

Wawili kati ya watoto hao mvulana na msichana, hali yao ya afya imeimarika lakini mvulana wa pili bado anapata matibabu ya matatizo ya upumuaji, katika hospitali moja jimbo la San Luis Potosí.

Msemaji wa kamati ya masuala ya afya, alisema magonjwa ya maambukizi kwa watoto wanaozaliwa bado haijawahi kutokea kokote kule duniani na hivyo basi hali hii inachunguzwa.

Ni idadi ndogo tu ya watoto wachanga ambao wamepata maambukizi ya virusi vya corona baada ya kuzaliwa, lakini maofisa wa afya wanaamini kwamba hali haikuwa hivyo kwa mapacha hao watatu.

Waziri wa Afya, Mónica Liliana Rangel Martínez, alisema: "Haiwezekani kwamba waliambukizwa wakati wanazaliwa"

Hata hivyo wazazi wao wanapimwa virusi vya corona huku mamlaka ikisema huenda ni wale wagonjwa wasioonesha dalili.

Mexico imerekodi maambukizi zaidi ya 185,000 ya virusi vya corona na vifo 22,584 tangu nchi hiyo iliporekodi mgonjwa wa kwanza wa virusi hivyo Februari 28 .

Virusi vya corona kwa watoto wachanga sio jambo la kawaida, kiasi kwamba haijawahi kutokea kabisa.

Watoto wanaweza kupata virusi vya corona baada ya kuzaliwa ikiwa watachangamana kwa karibu na yeyote ambaye tayari ameambukizwa virusi vya corona.

Virusi vya corona pia vinaweza kusambazwa hadi kwenye tumbo la uzazi kutoka kwa mama hadi kwa mtoto kupitia kondo la nyuma.

Watafiti Marekani kutoka Shule ya Tiba ya Yale hivi karibuni walitangaza maambukizi ya kwanza ya virusi vya corona kutoka kwa kondo la nyuma la mama.

Maambukizi yanapotokea, hatari ya kusambaa kutoka kwa mama hadi kwa mtoto iko chini, ingawa baadhi ya utafiti unaonesha kwamba yanaweza kuongeza uwezekano wa watoto kuzaliwa kabla ya muda.

***BBC***

# Burundi wapata Waziri Mkuu kwa mara ya kwanza

**BUJUMBURA, Burundi**

BUNGE la Burundi juzi liliidhinisha uteuzi wa Makamu Rais na Waziri Mkuu, ambao walipendekezwa na Rais mpya, Evariste Ndayishimiye.

Prosper Bazombanza kutoka chama cha UPRONA aliidhinishwa kuwa Makamu wa Rais kwa kura 91.

Naye Alain-Guillaume Bunyoni, Ofisa mwenye cheo cha juu katika Jeshi la Polisi, ambaye pia aliwahi kuwa Waziri wa Usalama wa serIkali inayoondoka madarakani, alipitishwa kwa kura 94 za wabunge, kama Waziri Mkuu mpya.

Cheo cha Waziri Mkuu ni kipya, kwa mujibu wa katiba mpya ya Burundi. Katiba hiyo pia imeondoa cheo cha mmoja wa Makamu wa Rais, kwani katiba ya zamani ilitambua makamu wawili wa rais.

Bazombanza aliwahi kuhudumu kama makamu wa kwanza wa rais chini ya uongozi wa Rais wa zamani aliyefariki, Pierre Nkurunziza, kuanzia mwaka wa 2014 hadi 2015.

Bunyoni yupo chini ya vikwazo vya Marekani na Umoja wa Ulaya kwa tuhuma za ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu, wakati wa maandamano ya April 2015, ya kupinga muhula wa tatu wa Rais Nkurunziza.

Wakati huo huo, habari ambazo hazijathibitishwa zinaeleza kwamba mwili wa rais wa zamani, Pierre Nkurunziza, utazikwa kesho katika mji wa Gitega, ulio takriban Kilomita 60 Mashariki mwa Bujumbura.

**VOA**

**Cheo cha Waziri Mkuu ni kipya, kwa mujibu wa katiba mpya ya Burundi. Katiba hiyo pia imeondoa cheo cha mmoja wa Makamu wa Rais, kwani katiba ya zamani ilitambua makamu wawili wa rais.**



Mwanasiasa wa upinzani nchini Uganda, Bobi Wine, ambaye anatajwa kuwa mshindani wa Rais Yoweri Museveni kwenye uchaguzi mkuu mwakani. **PICHA; REUTERS**

# Iran iko tayari kwa mazungumzo endapo Marekani itaomba radhi

**TEHRAN, Iran**

RAIS wa Iran, Hassan Rouhani, amesema nchi yake iko tayari kufanya mazungumzo na Marekani, iwapo Marekani itaomba msamaha pamoja na kuilipa Iran fidia, kutokana na kujitoa katika mkataba wa nyuklia wa mwaka 2015.

Uhasama kati ya Marekani na Iran, umeongezeka tangu mwaka 2018 wakati Rais wa Marekani, Donald Trump, alipoiondoa nchi yake katika mkataba wa nyuklia uliosainiwa baina ya Iran na mataifa makubwa yaliyo na nguvu duniani mwaka 2015, baadae kuiwekea Jamhuri hiyo ya kiislamu vikwazo vilivyouathiri uchumi wake.

"Hatuna tatizo lolote la kuwa na mazungumzo na Marekani, lakini hilo litafanyika iwapo Marekani itatekeleza wajibu wake juu ya mkataba wa nyuklia, iombe msamaha na itulipe fidia kwa kujitoa katika mkataba huo wa mwaka 2015," alisema Rais Rouhani na kuongeza:

"Lakini tunajua hii miito ya kutaka mazungumzo na Iran inayotolewa na Mmarekani ni ya uwongo mtupu," alisema Rouhani katika hotuba iliyorushwa moja kwa moja kupitia televisheni ya kitaifa.

Iran imekataa kuwa na mazungumzo ya aina yoyote na Marekani ambayo inajaribu kuishinikiza kuwa na mpango mpya, hadi pale itakapoiondolea vikwazo na kurejesha mezani makubaliano yaliyoidhinishwa awali.

Katika ujumbe aliouandika katika mtandao wake wa Twitter mapema mwezi huu, Rais Trump alirejelea msimamo wake wa kutaka mpango mpya na Iran, unaonuiwa kudhibiti shughuli za kinyuklia, kusitisha mpango wake wa makombora ya masafa marefu na kumaliza vita vyake vya chini kwa chini na Marekani vilivyodumu kwa miongo kadhaa.

Katika kujibu sera ya Marekani ya kushinikiza kupata inachokitaka, Iran inaendelea kukiuka makubaliano yaliyoko katika mkataba wa nyuklia juu ya kupunguza shughuli zake za nyuklia, lakini imesema inaweza kuanza kutii tena makubaliano hayo iwapo washirika wengine wa Ulaya katika mkataba huo watatekeleza ahadi yao ya kuilinda Iran kutokana na adhabu ya kiuchumi iliyowekewa na Marekani.

***DW***

# Vyama vya Upinzani Uganda vyaigomea Tume ya Uchaguzi

**KAMPALA, Uganda**

VYAMA vya upinzani nchini Uganda vimekataa mpangilio mpya uliotangazwa na Tume ya uchaguzi nchini humo kuwa, kampeni zote zifanyike kupitia vyombo vya Habari na mitandao ya kijamii kuelekea uchaguzi mkuu mwakani.

Robert Kyagulanyi maarufu kama Bobie Wine ambaye ni kiongozi wa kundi la 'People Power' na mgombea wa zamani wa urais, Dk.Kizza Besigye na chama chake FDC wamepinga mpango huo.

Tume ya uchaguzi nchini Uganda na chama tawala cha NRM walisema kwamba mpango huo ni mzuri kwa kutimiza katiba na uchaguzi, lakini pia kulinda mamilioni ya wananchi dhidi ya maambukizi ya ugonjwa hatari wa corona.Uganda imerekodi visa 797 vya maambukizi ya ugonjwa wa corona baada ya visa vipya 19 kuthibitishwa, huku wagonjwa 699 wakithibitishwa kupona ugonjwa huo.

Rais wa nchi hiyo, Yoweri Museveni aliwasihi wananchi kukumbatia mpango huo, huku akionya kwa yeyote atakayehatarisha usalama wa taifa kwa vurugu.

Tume ya Uchaguzi inaendelea na mpango wa kuandaa uchaguzi lakini wapinzani wanasema uchaguzi huo ni kinyume na katiba na kushtumu kwamba kuna njama za kumpa ushindi Rais Yoweri Kaguta Museveni.

***RFI***




# SANCHO

## AKOLEZA MOTO USAJILI UNITED

**DORTMUND, Ujerumani**

JADON Sancho amewapa matumaini mashabiki wa Manchester United huenda akajiunga na klabu hiyo wakati wa usajili wa majira ya joto, akitokea Borussia Dortmund ya Ujerumani.

Sancho ametoa matumaini yao kwa mashabiki wa Manchester United, baada ya kubonyeza kitufe cha 'like' kwenye posti ya Twitter iliyoandikwa "Akili yake tayari ipo Manchester United."

Kiungo huyo wa kimataifa wa England aliwekwa benchi katika mchezo uliopita wa Ligi Kuu Ujerumani, wakati klabu yake ya Borussia Dortmund ilipoifunga RB Leipzig mabao 2-0.

Jambo hilo liliibua minong'ono kwamba winga huyo mwenye umri wa miaka 20, ameshawekwa kando kwenye kikosi hicho kutokana na akili yake kufikiria kuondoka.

Mtangazaji wa mashindano ya mbio za magari za Formula I huko Ujerumani, Heiko Wasser aliandika Twitter kuhusu Sancho kuwekwa benchi, aliposti: "Akili yake tayari ipo Manchester United."

Mashabiki wa United walichukua posti hiyo na 'kushea' kwenye mitandao ya kijamii, jambo lililokuja kuwafurahisha zaidi baada ya Sancho mwenyewe kuweka 'like' kwenye posti inayodai kwamba akili yake ipo Old Trafford.

Shabiki mmoja aliandika: "Akili yake tayari ipo Manchester United. Nasubiri kwa hamu kumwona kwenye kikosi cha United."

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Michezo wa Dortmund, Michael Zorc amesema Sancho aliwekwa benchi kwenye mechi ya Leipzig kwa sababu ya uchovu na si kufikiria kuachana na klabu hiyo.

***

# VIRGIL MATUMAINI KIBAO LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

MLINZI wa kati wa Liverpool, Virgil van Dijk, amewaonya wapinzani wao kuwa timu yao ndio kwanza inaanza kutawala soka la England na wanatarajia watatamba kwa miaka kadhaa ijayo.

Liverpool chini ya kocha Jurgen Klopp ilimaliza nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu ya England msimu uliopita na kutwaa Ligi ya Mabingwa Ulaya na klabu kubwa ya dunia, na sasa inaelekea kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu kwa mara ya kwanza baada ya kupita miaka 30.

"Tunatumaini tupo katika hali nzuri ya kumalizia kazi tuliyoianza. Kitu cha muhimu zaidi maishani ni afya na sote tulilazimika kukabiliana na kusimamishwa kwa ligi," alisema Van Dijk akinukuliwa na Sky Sport.


Van Dijk alituma ujumbe kwa mashabiki kuwa, licha ya kuwa kileleni kwa tofauti ya zaidi ya pointi 22, ndio kwanza wanaanza safari ya kulitawala soka la England.

"Najua ni kwa muda gani mashabiki wamesubiria mafanikio haya. Lakini bahati mbaya hawawezi kuwapo kama itatokea tumetwaa ubingwa.

"Tukishinda mechi mbili tu sisi ni mabingwa, lakini hatutaishia hapo. Tunataka kuendelea mbele, tunataka kulibakiza kombe hata msimu ujao ambao utaanza haraka baada ya mechi ya mwisho ya msimu huu.

Kocha ameshatuambia kwamba, tutakachokifanya kwenye mechi tisa zilizobaki, kitatupa mwongozo kuelekea msimu ujao.

Tunataka kuendelea kujiboresha. Tuna wachezaji ambao wanaweza kuwa bora zaidi. Kama tukitwaa ubingwa, tutataka kuutetea msimu ujao.



# AUBAMEYANG AONYWA KUONDOKA ARSENAL

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Arsenal, Ian Wright amemwonya straika wa Washika Bunduki hao Pierre Emerick Aubameyang, kuhusu kufikiria kutaka kuondoka ndani ya klabu hiyo.

Ripoti zimebainisha kwamba, Aubameyang ana mpango wa kuondoka ndani ya Arsenal huku AC Milan, Real Madrid na Barcelona zikitajwa kuwania saini yake.

Mkataba wake wa sasa na Arsenal unamalizika mwishoni mwa msimu ujao na hadi sasa mazungumzo juu ya kusaini mkataba mpya yamekwama.

Na sasa fowadi wa zamani wa Arsenal ambaye alicheza msimu wa 1991 hadi 98, akicheza jumla ya mechi 221 na kutupia mabao 128, amesema kuwa akiendelea kuwasumbua Arsenal atapotea.

Nyota huyo amesema kuwa anatambua malengo ya Aubameyang ni kucheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ili kufikia hayo ni lazima awe na subira kwani nafasi yake ya kufanikiwa ndani ya Arsenal ni kubwa.

"Mkataba ambao anapewa na Arsenal ni mkubwa na anapaswa auheshimu akisema alete jeuri anaweza kushangaa anaanza kuchezea benchi labda Kocha Mikel Arteta anaweza kumpa nafasi (Gabriel) Martinelli, yeye atafunga lini?" Alisema akinukuliwa na Sky Sport.

Hadi sasa hatima ya mshambuliaji huyo raia wa Gabon bado haijajulikana ndani ya klabu hiyo.





# MFUMO WA MOURINHO KUMKIMBIZA KANE

**LONDON, England**

MFUMO wa Kocha Jose Mourinho pale Tottenham Hotspur umedaiwa unaweza kusababisha kumpoteza straika wao, Harry Kane.

Kwa mujibu wa kiungo wa zamani wa England, Paul Merson, Kane anaweza kuanza kufikiria namna ya kwenda kujiunga na timu itakayompa nafasi ya kushambulia kuliko kuendelea kubaki kuwa chini ya mfumo wa Mourinho, anayezingatia zaidi kujilinda kuliko kwenda kushambulia.

Kane alionekana kutokuwa kwenye kiwango chake Ijumaa iliyopita kwenye sare ya 1-1 dhidi ya Manchester United katika mchezo wa Ligi Kuu England, kwa sababu Mourinho aliweka wachezaji wa kujilinda tu kwenye kikosi chake hicho.

Kane, aliyewahi kushinda kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu England mara mbili, alishawahi kuhusishwa na Manchester United, huku mwenyewe akidai anaweza kufikiria kuondoka kama Spurs haitakuwa na uwezo wa kumpa mataji.

"Jose alipochukua kazi ya kuinoa Spurs nilipata wasiwasi juu ya Harry Kane," alisema staa huyo wa zamani wa Arsenal.

"Walicheza na watu 10 tu uwanjani. Sikumbuki hata aligusa mpira mara ngapi kwenye mechi yote."



# MAJERUHI YA AGUERO YAMTISHA GUARDIOLA

**MANCHESTER, England**

MSHAMBULIAJI Sergio Aguero huenda ameumia kwa kiasi kikubwa goti lake katika mchezo dhidi ya Burnley mwishoni mwa wiki, kwa mujibu wa kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.

Mshambuliaji huyo wa Argentina alicheza kwa dakika 45 tu kwenye mchezo huo dhidi ya Burnley na baada ya hapo akaumia na nafasi yake kuchukuliwa na Gabriel Jesus.

Guardiola alisema: "Haonekani kuwa sawa, goti lake lina tatizo, tutaona kesho (Jumanne), baada ya uchunguzi. Alikuwa akipambana tangu mwezi uliopita kuhusu maumivu katika goti lake, tutaona."

Alipoulizwa ikiwa ana wasiwasi Aguero atakosa msimu wote, Guardiola alijibu itategemeana na vipimo vya mwisho.

"Kesho tutaona. Mimi sio daktari, lakini haonekani kuwa sawa," alisema Guardiola.

Kuumia kwa Aguero kunaiweka City katika wakati mgumu kwenye harakati zao za kuwania mataji tofauti wanayoshiriki msimu huu.

Wakati wakiwa na uwezekano finyu wa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England, City bado wapo katika mbio za kuwania mataji mawili ambayo ni Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA.

Ikumbukwe tayari msimu huu, City wameshatwaa taji moja ambalo ni Kombe la Ligi. Taji hilo walitwaa Machi, mwaka huu baada ya kuifunga Aston Villa anayoichezea nahodha wa Tanzania, Mbwana Samatta kwenye Uwanja wa Wembley.

# KIPA UNITED KUONGEZA MKATABA SHEFFIELD

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Sheffield United, Chris Wilder anaamini klabu yake ipo karibu zaidi kuurefusha mkataba wa mkopo wa mlinda mlango wa Manchester United, Dean Henderson.

Dean ambaye ana umri wa miaka 23, amekuwa nguzo muhimu ndani ya kikosi cha Sheffield ambacho kimeonyesha kiwango kikubwa katika msimu huu wa kwanza baada ya kupanda daraja.

Mkataba wake wa mkopo unatarajia kufikia tamati Juni 30, mwaka huu na tayari mazungumzo baina ya klabu hizo mbili yameanza ili kuangalia uwezekano wa kurefusha hadi pale msimu utakapomalizika.

Wilder alisema wana matumaini ya kuendelea na Henderson, lakini amri ya mwisho iko mikononi mwa United ambayo ndio inammiliki mchezaji huyo.

"Naamini kuwa, kwa sasa maamuzi yapo kwa viongozi wa klabu zote mbili, lakini nimekuwa naongea na Ole Gunnar Solskjaer na ameonyesha kukubali kuwa mchezaji huyu asalie hapa hadi mwisho wa msimu na tuna imani kuwa tutamsainisha mapema kabla ya mkataba wake kufikia siku za mwisho.

Nathamini mchango wa Ole na kwenye suala hili, naamini kuwa Dean ni bora kwao na sisi pia ni bora kwetu," alisema Wilder.

Henderson amekuwa na kiwango bora msimu huu akiwa na kikosi cha Sheffield ambapo katika michezo 29 aliyoichezea timu hiyo kwenye Ligi Kuu, hajaruhusu nyavu zake kutikiswa katika michezo 11.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LUIZ KUENDELEA KUPETA ARSENAL

●●●Klabu hiyo yampatia mkataba mpya wa mwaka mmoja licha ya kiwango cha beki huyo Mbrazil ...

**LONDON, England**

KATIKA hali ya kushangaza, David Luiz amekubali kusaini mkataba mpya wa mwaka mmoja wa kuendelea kuitumikia Arsenal.

Pia mchezaji mwenzake, Cedric Soares amekubali kusaini mkataba mpya wa kudumu wa miaka minne wa kukaa klabuni hapo akitokea Southampton kwa mkopo.

Beki huyo wa kati kutoka Brazil, alianzisha mjadala mkubwa na kulalamikiwa kutokana na kiwango kibovu alichokionyesha katika mechi dhidi ya Manchester City iliyochezwa wiki iliyopita na kutolewa nje dakika ya 26, huku akiiacha timu yake ikiambulia kichapo cha mabao 3-0 kwenye mchezo huo.

Luiz alilazimika kuomba radhi kutokana na malalamiko yaliyopelekwa kwake na ilionekana kama huo safari yake ndani ya Arsenal itaishia mwisho wa msimu huu, baada ya mkataba wake unaomalizika Juni 30, mwaka huu ambao analipwa mshahara wa pauni 120,000.

Hadi Jumanne usiku, klabu ilikuwa inapambana kuhakikisha anasaini mkataba mfupi ambao utamweka klabuni hapo hadi mwisho wa msimu, lakini baadaye Arsenal imeamua kumpa mkataba mrefu ambao utamfanya Luiz aitumikie timu hiyo hadi 2021.

Mikel Arteta amefanya hivyo baada ya kuelewa umuhimu wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 33, pamoja na beki wa kulia, Soares, ambaye alijiunga kwa mkopo Januari mwaka huu, lakini hajacheza mechi hata moja.

Soares amekuwa akisumbuliwa na maumivu ya mguu, lakini Arteta amevutiwa na nyota hao wawili kutokana na wanavyojituma mazoezini na anaamini watakuwa na mchango mkubwa kwenye timu siku za usoni.

Pia beki, Pablo Mari, ambaye yuko nje ya uwanja wa miezi minne kutokana na majeraha ya kifundo cha mguu, naye amesaini mkataba wa kudumu. Mari alijiunga kwa mkopo akitokea Flamengo.

Gazeti la Sportsmail la wiki iliyopita liliandika ada ya Mhispania huyo mwenye umri wa miaka 26, ni pauni milioni 14. Wakati huo huo, Arteta amefungua milango ya kuondoka klabuni hapo kwa Matteo Guendouzi kwa sababu ya kiungo huyo kutojielewa, akionekana akifanya vitendo visivyokuwa na nidhamu kwenye kamera wakati wa mazoezi.

Guendouzi ameanza katika mechi mbili kati ya michezo 10 chini ya Arteta, huku pia ikielezwa straika Gabriel Martinelli atakuwa nje kwa muda wa mwezi mmoja baada ya kuumia mazoezini Jumapili.

## KWA UFUPI

### ARTHUR ANUKIA JUVENTUS
JUVENTUS imekubali kulipa ada ya pauni milioni 72.5 ili kumsajili nyota wa Barcelona, Arthur (22), lakini italazimika kumshawishi kiungo huyo Mbrazil kukubali kujiunga na klabu yao. ***(Sky Sports)***

### CARVALHO KUTUA LEICESTER
KIUNGO Mreno, William Carvalho (28), amefikia makubaliano binafsi na Leicester City, na sasa klabu hiyo ya Ligi Kuu England inatakiwa kukubali kulipa ada ya uhamisho itakayotakiwa na Real Betis. ***(Marca)***

### PALACE KUMSAJILI FERGUSON
CRYSTAL Palace inakaribia kukamilisha mchakato wa kumsajili, Nathan Ferguson, baada ya beki huyo wa West Brom ambaye ana umri wa miaka 19, kukataa kusaini mkataba mpya na klabu yake. ***(Guardian)***

### ARSENAL, SOARES SAFI
ARSENAL inatarajia kuendelea kumtumia beki Mreno, Cedric Soares ambaye yuko kwa mkopo akitokea Southampton kwa kumpa mkataba wa kudumu wakati dirisha la usajili la majira ya joto litakapofunguliwa. ***(ESPN)***

### CARROLL KUBAKIA NEWCASTLE
STRAIKA raia wa England, Andy Carroll, ambaye ana umri wa miaka 31, anatarajia kusaini mkataba mwingine wa mwaka mmoja na klabu yake ya Newcastle United. ***(Chronicle)***

### MC-GHEE AGOMBEWA
KIUNGO wa Manchester United, ambaye ana umri wa miaka 19, Dion McGhee, anawindwa na klabu mbalimbali ikiwamo West Ham, Rangers na AZ Alkmaar. ***(Manchester Evening News)***

### ENGLAND YAJIPANGA
MAMLAKA za soka England zinajiandaa kuangalia uwezekano wa kuruhusu mashabiki katika mechi ya Ngao ya Jamii kama maandalizi ya kurejea kwa washangiliaji hao kabla ya kuanza kwa msimu mpya. ***(Times - subscription required)***

### ARSENAL KUMKOSA MARTINELL
KIUNGO wa Arsenal kutoka Brazil, Gabriel Martinelli, ambaye ana umri wa miaka 19, atakosa mechi zote za ligi zilizosalia msimu huu kwa sababu ya kupata majeraha ya mguu kwenye mazoezi ya timu hiyo. ***(Mirror)***

### SAN SIRO IMEKAMILIKA
KUNA hatua muhimu zinatarajiwa kuchukuliwa baada ya kukamilika kwa matengenezo kwenye Uwanja wa San Siro, baada ya kufanyika kikao kilichowahusisha, AC Milan, Inter Milan na wakurugenzi wa jiji ambao ndio wamiliki wa uwanja huo. ***(Gazzetta dello Sport - in Italian)***

### BADIASHILLE ANUKIA RENNES
MABOSI wa Rennes wamewasilisha ofa ya pauni milioni 13.55 kwa Monaco, ili kumsajili beki Mfaransa, Benoit Badiashile, ambaye ana umri wa miaka 19. ***(RMC Sport - in French)***

### JUVE BADO YAMTAKA JORGINHO
JUVENTUS inajipanga kumsajili kiungo wa Chelsea, Jorginho lakini changamoto ya fedha inaweza kuwa tatizo la kukwamisha mchakato huo kukamilika. ***(Express)***

### GOTZE KUTUA ATLETICO
ATLETICO Madrid imeweka wazi nia yake ya kumsajili kiungo wa Borussia Dortmund, Mario Gotze, ambaye anatajwa amekataa kusaini mkataba mpya na vigogo hao wa Bundesliga akimaanisha anataka kuondoka akiwa mchezaji huru ifikapo majira ya joto. ***(Bild)***

# YANGA YAUMIA KUMKOSA MORRISON LIGI KUU BARA

**Na Saada Akida**

BENCHI la Ufundi la Yanga linasikitika kumkosa mshambuliaji wake, Bernard Morrison katika mechi mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kusimamishwa na Shirikisho la Soka Tanzania, (TFF), imefahamika.

Kamati ya Nidhamu ya TFF, ilitangaza kumfungia Mghana huyo pamoja na kiungo wa Simba, Jonas Mkude na kulipa faini ya Sh. 500,000 kutokana na vitendo ambavyo si vya kiungwana katika michezo, tofauti ya Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, mmoja wa makocha wa Yanga, Said Maulid 'SMG' alisema taarifa za kutomtumia nyota huyo katika mechi mbili kutaiathiri timu yao ambayo inahitaji kufanya vizuri ili kumaliza kwenye nafasi ya pili katika msimamo.

SMG alisema wamepata taarifa hizo za kumtomtumia nyota huyo katika michezo miwili hali ambayo inatawathiri katika mipango yao.

"Alikuwapo katika mipango yetu ya mechi hizi mbili (Namungo na Kagera Sugar), lakini tumefika hapa (TFF), asubuhi tukaambiwa katika 'pre match meeting' taarifa hizo, alikuwa tegemeo katika michezo hiyo," alisema SMG.

Hata hivyo, mshambuliaji huyo wa zamani wa Yanga alisema nafasi yake itazibwa na mchezaji mwingine na watajipanga kuingia uwanjani kwa lengo la kuondoka na pointi tatu muhimu.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nidhamu ya TFF, Peter Heller, alisema Morrison amepewa adhabu hiyo kwa kumpiga kiwiko mchezaji wa Tanzania Prisons, huku Mkude akifanya kosa kama hilo kwa mchezaji wa Biashara United katika mchezo 223 wa Ligi Kuu Bara.

"Kuna mashauri 12 yaliletwa kwetu ikiwamo ya Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza, ambayo yalifanyika kabla ya kusimama kwa ligi hizo kutokana na janga la corona, mengine tuliyatolea maamuzi huku mengine tulishindwa kutokana na kutokamilika kwa ushahidi," alisema Heller.

Alizitaja kesi zilizokosa mashauri ni inayomhusu, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, Kocha wa Yanga, Luc Eymael na Kocha wa Namungo, Thierry Hitimana kwa madai ya kuchafua nembo ya shirikisho, yaliyoondolewa baada ya bodi kukosa ushahidi.




Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Nidhamu ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Peter Heller (kushoto), akitangaza uamuzi wa kamati hiyo kumfungia kiungo wa Simba, Jonas Mkude na mshambuliaji wa Yanga, Bernard Morrison kwa sababu ya kufanya vitendo ambavyo si vya kiungwana katika mechi za Ligi Kuu Bara. Kulia ni Mkurugenzi wa Sheria wa TFF, Rahim Shaaban. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kocha afunguka hatima Singida

**Na Adam Fungamwango**

NI kama jahazi la Singida United limeanza kuzama kwenye kina kirefu cha maji, baada ya juzi kuchapwa mabao 3-1 ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Liti, Singida ilipoikaribisha Mtibwa Sugar, huku Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ramadhani Nswanzurimo akisema hata wakishuka daraja, hawatasambaratika.

Nswanzurimo alisema walipoteza mechi hiyo kutokana na wachezaji ambao hawana uzoefu na Ligi Kuu, kushindwa kutumia vema nafasi za kufunga ambazo walizitengeneza katika mchezo huo.

"Lakini hii yote ndio soka, mpaka sasa hatujashuka daraja, lakini kumekuwa na maneno mengi ya kutubeza kuwa tutaporomoka. Ni hivi, hata kama Singida United itashuka daraja, lakini klabu itakuwapo, haitovunjika. Singida haitokuwa timu ya kwanza kwenye ulimwengu wa soka," alisema kocha huyo.

Singida United inaburuza mkia, ikiwa kwenye nafasi ya 20 kwa pointi 15 tu ilizokuwa nazo na iwapo ikishinda mechi zake saba ilizobaki nazo, itafikisha pointi 36, na kuwa bado kwenye nafasi isiyo salama.

Siku ya Jumamosi timu hiyo itakuwa tena na kibarua kizito, itakapokuwa nyumbani kwenye Uwanja wa Liti, ikiikaribisha Lipuli FC ya Iringa ambayo nayo imetoka kupokea kipigo kizito cha mabao 3-0 dhidi ya Mwadui FC kwenye Uwanja wa Mwadui Complex mkoani Shinyanga.

## Coastal Union yalia na mabeki

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA wa Coastal Union, Juma Mgunda, amesema safu yao ya ulinzi ilikuwa na mapungufu na hivyo kuruhusu timu yao kupoteza mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Alliance FC uliochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza hapo juzi.

Mgunda alisema hakuridhishwa na safu yake ya ulinzi katika mechi hiyo na ameahidi kuendelea kuifanyia kazi ili kuvuna ushindi katika mechi zinazofuata.

"Safu yangu ya kukaba ina shida kubwa, tayari nimeona na nitajitahidi kuifanyia kazi ya ziada ili iweze kuwa sawa," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema uzembe wa safu hiyo 'unampasua kichwa' kwa muda mrefu na kusema imesababisha kushindwa 'kufurukuta' mbele ya Mbao FC.

"Jana (juzi) tulishindwa kupata matokeo mazuri tulipokutana na Mbao FC kutokana na uzembe uliofanywa na wakabaji wangu, naahidi kufanya marekebisho ili kuitetea timu yangu," Mgunda alisema.

Aliongeza mchezo huo ulikuwa mgumu na ushindani na aliwapongeza wapinzani wao kwa kutumia vizuri nafasi walizotengeneza.

## Waluguru Original yakamilisha albamu

**Na Sabato Kasika**

BENDI ya muziki wa dansi ya Waluguru Original ya mkoani Morogoro, iko katika hatua za mwisho za maandalizi ya uzinduzi wa albamu mpya utakaofanyika mwezi ujao.

Akizungumza na gazeti hili, Mkurugenzi wa bendi hiyo, Deogratius David 'Killer Boy', alisema uzinduzi wa albamu hiyo utakuwa ni wa kwanza bendi hiyo mwaka huu.

Killer Boys alisema bendi imekamilisha nyimbo sita na baadhi yake tayari zimeshasambazwa kwenye vituo mbalimbali vya redio vya Morogoro ili kuitambulisha albamu mpya.

"Unajua wakati shughuli za burudani zinasimama kupisha maambukizi ya corona, tulikuwa tayari tumeandaa nyimbo za albamu mpya, tukalazimika kusimama kwa muda, lakini sasa tumeanza maandalizi upya.

Waluguru Original tuna nyimbo mpya za Morogoro Yetu, Mwanzo wa Mapenzi, Cha Kupewa, Ngalile Mwanangu Ndole, Supu na Nataka Nilewe', na tumeshasambaza redioni wimbo wa Morogoro Yetu," Killer Boy alisema.

Mkurugenzi huyo alifafanua huenda wimbo huo ndiyo ukabeba jina la albamu, kwa madai kwamba mashabiki wao wamekuwa wakiomba wapigiwe kila bendi hiyo inapofanya maonyesho yake mkoani humo. Alisema, mbali na kuendelea kurekodi nyimbo zao, pia wako kwenye mazungumzo na bendi moja kubwa ya jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kushiriki katika uzinduzi huo.

Michezo
Alhamisi Juni 25, 2020
Nipashe



## Luiz kuendelea kupeta Arsenal

HABARI UK 22




Mashabiki wa Simba wakishangilia baada ya timu yao kupata bao la kwanza katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mbeya City iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya. Simba ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# BOCCO ASOGEZA UBINGWA SIMBA

●●●Mabao yake mawili yaifanya Simba ibakishe pointi mbili tu ili kujitangazia rasmi ufalme kwa msimu wa tatu...

**Na Adam Fungamwago**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, wamekaribia kabisa kutwaa tena taji hilo kwa mara ya tatu mfululizo baada ya kuichapa Mbeya City mabao 2-0 kwenye mechi kali na ya kusisimua iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya jana.

Simba yenye pointi 78, inahitaji pointi mbili ili kufikisha pointi 80 ambazo haziwezi kufikiwa na timu nyingine kwenye ligi hiyo msimu huu, na kama itashinda mechi inayofuata dhidi ya Tanzania Prisons hapo Jumapili itafikisha pointi 81.

Hesabu hizo ni baada ya Azam FC jana kufungwa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar, hivyo kama itashinda mechi zake saba zilizobakia itafikisha pointi 78.

Yanga ambayo jana usiku ilitarajiwa kucheza dhidi ya Namungo kama ikishinda mechi zake zote nane ilizobaki, itafikisha pointi 79.

Mabao yote ya Simba katika mechi ya jana yalifungwa na nahodha wake, John Bocco, ambaye alianza kuwanyanyua mashabiki wa timu hiyo dakika ya tano, ambapo alimalizia mpira ulioanzia kwa Miraji Athumani na kupita kwa Chama, aliyeukokota mpira na kupiga krosi iliyounganishwa na mfungaji huyo hadi wavuni na kumwacha kipa, Aaron Kalambo asijue la kufanya.

Baada ya bao hilo Simba ilipoteana, hasa sehemu ya katikati na kuwapa mwanya viungo wa Mbeya City kutamba na kupeleka mashambulizi mfululizo kwenye lango la lao.

Dakika ya 29, mchezaji aliyeisumbua ngome ya Simba, Peter Mapunda alibaki yeye na kipa Manula, lakini alipiga shuti lililoloka nje kidogo ya lango.

Miraji Athumani nusura alipatie timu yake bao dakika ya 32, kama si uhodari wa kipa Kalambo kuudaka mpira kwa ustadi mkubwa.

Mbeya City itabidi ijilaumu yenyewe baada ya kukosa mabao mawili ya wazi, dakika ya 44, baada ya Abasalim Chidiebere kupiga shuti lililowachanganya mabeki wa Simba, kabla ya kurejea uwanjani na kumkuta George Chota aliyepiga shuti lililotoka pembeni kidogo ya lango.

Mabadiliko ya kuwatoa Francis Kahata na Said Ndemla na kuwaingiza, Luis Miquissone na Mzamiru Yassin, yalibadilisha kidogo kiungo cha Simba, na kuanza kupeleka mashambulizi ya uhakika langoni mwa Mbeya City.

Alikuwa tena yule yule, Bocco aliyefunga bao la pili dakika ya 53, baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Gerson Fraga kuwanyang'anya mpira wachezaji wa Mbeya City na kumpa Miraji aliyeunyanyua juu na kumkuta mfungaji aliyeudokoa kidogo na mpira kujaa wavuni, huku kipa Kalambo akiwa anatoka golini kumwahi mfungaji asipige.

Dakika za majeruhi, Miraji alipachika bao, lakini mwamuzi, Athumani Lazi alilikataa kwa madai kuwa mchezaji wa Mbeya City aliumizwa, muda mchache kabla ya kufunga goli hilo, ingawa aliumizwa na mchezaji mwenzake katika harakati za kuzuia mashambulizi kuelekea langoni mwao.

Ni mechi iliyohudhuriwa na umati mkubwa wa wa tu, ikishuhudia dakika ya kwanza tu Simba ikikosa bao la wazi, baada ya Claotus Chama kupiga hewa, akiwa kwenye nafasi nzuri ya kupachika bao.

Dakika ya tatu, Emamanuel Memba alipiga kona iliyokuwa ikimiminika wavuni, lakini kwa ustadi kipa wa Simba na Timu ya Taifa (Taifa Stars), Aishi Manula akaupangua na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Mjini Musoma, Mara wenyeji Biashara United walipata ushindi mnono wa mabao 4-0 dhidi ya KMC FC wakati kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza Alliance FC walitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania.

## YANGA, MORRISON FILAMU INAENDELEA

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI Yanga ikisisitiza ina mkataba na kiungo wake wa kimataifa Mghana, Bernard Morrison hadi Julai, mwaka 2022, klabu hiyo imetangaza kumkata faini ya Sh. milioni 1.5 katika mshahara wake.

Yanga ililazimika kutoa ufafanuzi baada ya juzi Morrison kukaririwa akisema mkataba wake na Yanga unamalizika mwezi ujao na hautambui mkataba mpya unaotangazwa na klabu hiyo.

Hata hizo taarifa ambazo zimepatikana jijini zinaeleza mkataba huo mpya wa Yanga, haujasajiliwa katika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), wala FIFA.

Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Simon Patrick alisema jana klabu hiyo iliingia mkataba mpya na Morrison ambao utamalizika Machi 20, 2022 baada ya kufikia makubaliano na nyota huyo ambaye mkataba wake wa awali wa miezi sita, ulikuwa unatarajiwa kumalizika Julai 14, mwaka huu.

Morrison alisema anafikiria kuondoka Yanga baada ya kutoridhishwa na baadhi ya mambo yanayoendelea katika klabu hiyo.

Naye Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kampuni ya GSM, ambao ni wadhamini wa klabu hiyo, Hersi Said alisema jana jijini kuwa Morrison ana mkataba halali na Yanga na alisaini baada ya kufikia makubaliano pande mbili hizo.

"Siku chake baada ya kusaini mkataba wa miaka miwili, alikuja (Morrison) kwangu yeye mwenyewe kuomba kuuvunja mkataba huo kwa sababu kuna timu imempa ofa nzuri ya mshahara wa Dola za Marekani 15,000, nilimjibu tayari mkataba umeshasainiwa hivyo kama anataka kuuvunja, klabu inayomtaka ifuate utaratibu kwa kuzungumza na Yanga," alisema Hersi.

Aliongeza mkataba huo aliushuhudia wakati kiungo huyo akisaini na waliusajili TFF na unatambuliwa kwenye mfumo wa FIFA.

Hata hivyo Nipashe ilibaini mkataba huo mpya haujawasilishwa TFF kwa kuwa utaratibu hauruhusu kusajili mkataba mpya wakati ule wa awali haujamalizika.

"Utaratibu wa kwenye 'system' (mfumo) wa kutambua mikataba ya wachezaji unakubali kuingiza mkataba mpya pale ule wa awali unapomalizika, lakini kuna vipindi maalum vya usajili, kwa sasa dirisha la usajili bado halijafunguliwa, kwa hiyo kwa suala hilo la (Morrison) mkataba unaosoma sasa hivi kwenye mfumo ni ule wa kwanza," alisema ofisa huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002